SportPesa
TZS. 667,771,400
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



RIPOTI MAALUM

**Mwanadada 'alivyotoka' kupitia kilimo mseto, alamba mamilioni**

UK. 4




**Moyo kumstaafisha soka Aguero**

UKURASA 22

Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Novemba 14, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0580765
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Machinga wavamia kanisani

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**ANWANI ZA MAKAZI KUKAMILIKA 2024**
WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji...

UKURASA WA 8
**MADHARA YA UMBEA NA MAJUNGU KATIKA FAMILIA**
TUNAISHI katika jamii ambapo ubinadamu unatawala hali ya ki-Mungu ndani...

## Majaliwa ashtukia mchezo mchafu misitu

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan, akikabidhi kifimbo cha Malkia kwa Mratibu wa Tanzania, Henry Tandau, kama ishara ya uzinduzi wa michezo ya Jumuiya ya Madola, katika hafla iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Samia awapoza machungu Stars

UKURASA 2

MICHEZO NABI AZICHAMBUA MECHI 'TATA' UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

## Majaliwa ashtukia mchezo mchafu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza wana-Iringa na Watanzania kwa ujumla wahakikishe wakati wanavuna miti wakumbuke kupanda miti mingi zaidi ili wapate faida zote zinazotokana na maliasili hiyo.

Vilevile ameonya mchezo mchafu unaofanyika kwenye mazao ya misitu unaohusisha miti ya Tanzania kuvunwa na kutengenezwa bidhaa ambazo zinaandikwa zimetoka nje ya nchi ilhali zimetokana na misitu ya Tanzania.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua Kongamano la Uwekezaji kwenye Sekta ya Misitu lililofanyika katika Viwanja vya Wambi vilivyopo Mji Mafinga, Iringa. "Mheshimiwa Rais amenituma niwaambie kuwa tunapovuna miti tuhakikishe tunapanda mingine ili kutunza mazingira," alisema.

Waziri Mkuu pia alitoa maelekezo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha sekta ya misitu ikiwa ni pamoja na kuzielekeza Wizara za Maliasili na Utalii na Wizara ya Viwanda na Biashara ziweke mazingira wezeshi ya kuvutia uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vya mazao ya misitu ili kuchakata mazao hayo kwa ufanisi na tija.

"Nitoe wito kwa wawekezaji kuja Iringa na kutumia vyema fursa za uwekezaji zilizopo kwenye miradi mikubwa ya mashamba ya miti na viwanda vya mazao ya miti. Viwanda hivyo vitasaidia kuepusha upotevu mwingi wa malighafi na kuwezesha kutumia mabaki yake kuzalisha bidhaa nyingine," alisema.

Majaliwa aliwaelekeza viongozi wa Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) waendelee kuwawezesha wajasiriamali wa misitu washiriki katika shughuli za misitu kwa kutoa ruzuku ili kuongeza kipato cha jamii.

Waziri Mkuu aliuelekeza uongozi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kushirikiana na mamlaka nyingine ikiwamo TAWA kuendeleza utatuzi wa migogoro iliyopo baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa.

Waziri Mkuu pia alielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii iweke mazingira mazuri yatakayowezesha sekta hiyo kuzalisha ajira nyingi zaidi kupitia mazao mbalimbali yatokanayo na maliasili hiyo kama ufugaji wa nyuki.

Majaliwa alisema ni muhimu kuendeleza utekelezaji wa mikakati ya kuwanufaisha wananchi wanaoishi jirani na misitu kupitia miradi ya ufugaji nyuki ikiwamo kutoa elimu kwa vikundi vya wafugaji nyuki na mafundi seremala.

Waziri Mkuu alizielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara zishirikiane katika kufatuta masoko ya mbao nje ya nchi.

Alimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu-Uwekezaji ahakikishe bidhaa zinazozalishwa katika viwanda mbalimbali nchini vikiwamo vya plywood zinawekwa nembo inayoonyesha kuwa zimezalishwa nchini.

"Lazima bidhaa hizo zionyeshe maeneo zilikozalishwa," Majaliwa aliagiza huku Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Geoffrey Mwambe, akisema wizara anayoiongoza kwa kushirikiana na wadau wa uwekezaji, itahakikisha vikwazo vyote vinavyowakabili wawekezaji nchini vinatafutiwa ufumbuzi.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, alisema pamoja na mambo mengine, kongamano hilo la siku tatu linalenga kuwakutanisha wadau wa sekta ya misitu ili kuongeza thamani katika mazao ya misitu pamoja na kutangaza fursa za uwekezaji kwenye sekta hiyo, hivyo kuongeza tija kwa mkoa.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizindua mwongozo wa kitaifa wa mazao ya mbao yaliyohandisiwa, katika kongamano la uwekezaji wa sekta ya misitu, mjini Mafinga, wilayani Mufindi, mkoani Iringa jana. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Geoffrey Mwambe (kushoto), Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (wa pili kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga. **PICHA: OWM**

# Machinga wavamia kanisani

**Na Mary Geofrey**

MAKAMU Askofu wa Kanisa la Orthodox, Jimbo la Dar es Salaam, Cleophace Bachuba, ameiomba Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam kuwaondoa wafanyakazi wadogo, maarufu machinga, wanaodaiwa kuvamia eneo la kanisa baada ya kuondolewa katika maeneo yasiyo rasmi.

Kiongozi huyo wa kiroho amesema wafanyabiashara hao walivamia eneo la kanisa na kuanza kujenga vibanda na wengine kugeuza sehemu ya kuhifadhi bidhaa zao, kitendo kinachowafanya washindwe kushiriki vyema ibada.

Askofu Buchuba alitoa ombi hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kikwazo anachopitia baada ya machinga hao kulitumia eneo hilo kufanya biashara.

"Eneo hili la kanisa lilikuwa ekari tatu lakini wakalimega hadi likabaki nusu ekari ambayo na yenyewe imevamiwa na hawa machinga wanaofanya biashara hadi nje ya eneo la kuingilia kanisani na kusababisha tunakosa sehemu ya kupita na gari," alilalamika Askofu Bachuba. Aliomba serikali kuwaondoa machinga hao ambao tayari wameanza kujenga vibanda vyao katika eneo hilo ili wawahamishie katika maeneo rasmi yaliyotengwa kwa ajili ya kufanya biashara zao.

Paroko wa Kanisa hilo, Padri Frumentios Msuri, alisema mara baada ya wafanyabiashara hao kuondolewa kwenye maeneo yasiyo rasmi, walijazana katika eneo hilo, wakilizunguka kanisa hali iliyowalazimu kuanza kujenga uzio.

"Tumeshajenga ukuta upande huu wa mbele ya kanisa, bado upande wa kulia ambako sasa ndiko wamejazana, hata ukitaka kuingia na gari hupati pa kuingilia, labda waanue kwanza biashara zao," alilalamika.

Alisema eneo hilo walipatiwa na mmoja wa waumini na kujenga kanisa mwaka 1939 na wamekuwa wakiendesha ibada zao miaka yote.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Salasala, Robert Massawe, alikanusha wananchi hao kuvamia eneo la kanisa, akidai kuwa eneo hilo ni la wazi na limekuwa likitumiwa kama njia ya wapita kwa miguu.

Alisema katika mtaa wake, kuna machinga zaidi ya 2,000 na eneo la Kisanga lililotengwa kwa ajili ya kufanyia biashara zao halitoshi, hivyo waliamua kuwaruhusu kufanya biashara pembeni ya kanisa hilo.

"Diwani anapambana sasa hivi ili kupatikane choo, tukimaliza kujenga, machinga hawa watatolewa na kwenda kupangwa katika eneo hilo, wala hakuna tatizo," alisema.

Mwenyekiti wa machinga hao, Kizito Ponsiano, alisema wafanyabiashara hao zaidi ya 200 hawafanyi biashara zao katika eneo la kanisa, bali wapo katika eneo la serikali.

Hata hivyo, alisema wanauomba uongozi wa kanisa hilo kuwapatia vielelezo vinavyoonyesha kuwa eneo hilo ni mali ya kanisa na kwamba wakiviona na kujiridhisha, wataondoka na kutafuta eneo lingine.

# Rais Samia awafuta machozi Taifa Stars

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameiagiza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, kusimamia kikamilifu maandalizi ya kushiriki michezo ya Jumuiya ya Madola ili nchi irejeshe medali ilizozipoteza kwa muda mrefu.

Aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam mara baada ya kupokea Kifimbo cha Malkia, ikiwa ni kiashirikia cha kuanza kwa michezo hiyo inayotarajiwa kufanyika Uingereza kuanzia Julai mpaka Agosti, mwakani.

Kifimbo hicho kiliwasili Dar es Salaam na leo kitaelekea visiwani Zanzibar na baadaye nchini Malawi.

"Turudishe uso wa Tanzania urudi, nuru ya Tanzania ionekane, wito wangu kwa wana michezo na walimu watakaochaguliwa kushiriki michezo hii, wahakikishe wanajituma na kuonyesha weledi wakapambanie taifa letu," aliagiza.

Alisema Tanzania imekuwa mwanachama na mshiriki mzuri wa michezo hiyo bila kukosa tangu mwaka 1962.

"Tumeshinda medali 21, kati yake sita za dhahabu, sita za fedha na tisa za shaba. Ninatambua Tanzania katika michezo ya Jumuiya ya Madola haijawahi kurudi bila kupata medali tangu tumeanza kushiriki, isipokuwa miaka mitatu 2010, 2014 na 2018 mfululizo," alisema.

Rais alisema hiyo ni mara ya saba tangu kifimbo hicho cha Malkia kuja Tanzania na alishiriki kukipokea akiwa Makamu wa Rais lakini washiriki walipokwenda waliiangusha nchi.

Aliiagiza Kamati ya Olimpiki iwasilishe mipango yake wizarani mapema ili ijadiliwe na hatimaye uangaliwe uwezekano wa kuingizwa kwenye mipango ya bajeti ijayo.

Alisema ujio wa kifimbo cha Malkia ambacho kina kamera inayoonyesha kodi kilikopita ni fursa kubwa kwa nchi kujitangaza na kujitambulisha duniani.

"Ninaiagiza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, na hili ninatoa kwa mtu ambaye ndiye, Dk. Hassan Abbas (Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo), kwa sababu hii kazi anaifanya vizuri, ameifanya vizuri kwenye Royal Tour, anaendelea na ataendelea kufanya tena, katika maeneo mengine.

"Ninavikumbusha vyama vingine vya michezo kuwa wabunifu, kuwaandaa wachezaji wao ili yasijirudie yaliyotokea Japan ambapo walipeleka wachezaji wa mbio ndefu pekee, mengine Rais wa Olimpiki ameomba tukutane hapa, tutasemana tutakapokutana," alisema.

TAIFA STARS

Kuhusu timu ya taifa ya wanaume (Taifa Stars), Rais Samia aliwataka wasife moyo kwa kutokana na kipigo cha mabao 3-0 walichokumbana nacho wiki hii nyumbani dhidi ya DR Congo kwa kuwa bado wanayo nafasi ya kushinda mechi ijayo na kuipa heshima nchi.

"Hata kama tutakuwa kwenye nafasi ya pili siyo mbaya, ninampongeza Waziri Mkuu, Wizara ya Michezo, TFF wachezaji na Watanzania, niliona ari na hamasa kuelekea mechi ya DR Congo, tulijipanga vizuri lakini bahati haikuwa yetu," alisema.

HABARI KITAIFA

## Uzalishaji mazao waongezeka JKT

Na Renatha Msungu, MOROGORO

UZALISHAJI wa mazao ya kilimo umeongezeka kutoka ekari 4,000 hadi 12,500 katika vikosi vya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Mkakati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, katika kikosi cha 837KJ Chita wakati akielezea mafanikio ya jeshi hilo katika kipindi cha miaka 60 tangu uhuru wa Tanzania Bara.

Alisema kumekuwa na ongezeko la uzalishaji ambapo kabla walikuwa wanazalisha katika ekari 4,000 lakini hadi katika msimu wa mwaka jana walifikisha ekari 8,517.

Hata hivyo, alisema katika msimu uliokwisha waliongeza kutoka ekari 8,517 hadi 14,300 na kwamba matarajio ni kulima ekari 26,000 katika mashamba yote ya vikosi vya JKT.

"Mfano, hapo nyuma kama shamba la Chita walikuwa wanavuna wastani wa magunia matatu hadi manne kwa ekari lakini tumetoka huko na kufikia magunia 10 kwa ekari moja," alisema.

Brigedia Jenerali Hassan Mabena ambaye pia ni MKuu wa Utawala wa JKT, alisema kwa namna wanavyoendelea kufuata taratibu za utaalamu wa kilimo, uzalishaji kwa ekari moja utaongezeka hadi magunia 30 ifikapo mwaka 2025 katika mazao yote ya mahindi, mpunga na maharagwe.

Alisema mkakati huo umewezesha kuzalisha magunia ya mahindi 39,000 ambayo yatatosheleza mahitaji ya zao hilo kwa vijana wa kujitolea kwa mwaka mzima.

"Lakini kidogo kwa mahindi tumefikia lengo, tukichukua mahindi yote ya vikosi tumeweza kupata magunia zaidi 39,000 na vijana wa kujitolea walioko kambini baada ya kufanya hesabu, wanatumia kwa mwaka nzima magunia 32, 000," alisema.

Brigedia Jenerali Mabena alisema ziada hiyo wataelekeza katika taasisi zingine za serikali kwa namna ambavyo yatahitajika lakini lengo la JKT ni kuhakikisha kuwa itakapofika mwaka 2024/25 waweze kutoa huduma kwa vijana wanaokuwa katika kambi.

Mkuu wa Kikosi cha 837KJ Chita, Luteni Kanali Evergreen Baltazary, alisema vijana ndio wanashiriki katika shughuli mbalimbali zinazofanywa katika kikosi hicho ambazo ni kilimo na ujenzi wa miundombinu ikiwamo ya umwagiliaji.

# Mwongozo waiva wahalifu wanaokimbilia Tanzania

Na Romana Mallya

MWONGOZO wa sheria utakaofuatwa na serikali za nchi za nje katika kupatiwa taarifa za raia wao waliokimbilia Tanzania baada ya kufanya uhalifu umezinduliа.

Akizindua mwongozi huo juzi jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, alisema kwamba kwa muda mrefu baadhi ya nchi zimekuwa zikipatiwa taarifa za wahalifu wa nchi zao waliopo Tanzania lakini wamekuwa wakikwama kutokana na maombi yao kutoendana na matakwa ya nchi.

Mwongozo huo umetengenezwa na Ofisi ya DPP kwa ufadhili wa Serikali ya Uingereza na Umoja wa Ulaya (EU).

DPP Mwakitalu alisema mwongozo huo utazisaidia nchi zinazohitaji kupatiwa taarifa za uhalifu au kuwakamata na kuwapeleka katika nchi zao.

"Katika uhusiano wa kimataifa inatakiwa kama mhalifu amefanya kosa nchi moja, akakimbilia nchi nyingine, lazima nchi husika aliyokimbilia itoe ushirikiano," alisema.

Kiongozi huo aliwataka wahalifu kuacha kutenda uhalifu kwa kuwa serikali na nchi nyingine zipo macho kukabiliana na uhalifu wa kila aina.

Balozi wa Uingereza nchini, David Concar, alisema jambo hilo lina umuhimu mkubwa kwa sababu mamilioni ya watu duniani wameathiriwa na matukio ambayo yanahusisha taifa moja na lingine pamoja na kuongezeka kwa ugaidi na rushwa.

"Tanzania ina nafasi kubwa kushiriki katika mapambano haya ili kukomesha vitendo hivi katika ngazi za kimataifa," alisema balozi huyo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akifungua pazia kuzindua Madrasatul-Maryam, iliyopo Mfenesini, Wilaya ya Magharibi "A ", Mkoa wa Mjini Magharibi jana. Kushoto ni Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said na Mwalimu Mkuu wa madrasa hiyo, Sheikh Hemed Suleiman. **PICHA: IKULU**

# Anwani za makazi kukamilika 2024

Na Paul Mabeja, DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, amesema serikali imepanga kuwa hadi ifikapo mwaka 2024, kila mwananchi anakuwa na anwani yake ya makazi.

Dk. Kijaji alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati akifungua semina ya uelewa wa pamoja kwa wakuu wa mikoa kuhusu mpango wa usambazaji wa mfumo wa anuani za makazi nchini.

Alisema hivi sasa serikali ipo katika utekelezaji wa mpango wa usambazaji wa anwani za makazi katika mikoa yote ili kurahisisha utoaji wa huduma katika maeneo mbalimbali ya nchi.

"Mfumo huu ndugu zangu wakuu wa mikoa unakwenda kutuondoa kwenye utaratibu wetu wa kusema nishushe hapo kwenye daraja au unapomweleza mtu unasema pale baada ya mbuyu mkubwa na siku hiyo mbuyu mkubwa ukikatwa itakuweje?"alihoji Dk. Kijaji.

Alisema anwani za makazi katika ulimwengu wa sasa ni jambo muhimu kutokana na ukuaji wa teknolojia, hivyo ni wajibu wa kila mkuu wa mkoa kuhakikisha kuwa mpango huo unafanikiwa.

"Anuani hizi zinakwenda kutoa majibu yote kwa kuweka majina ya mitaa, namba za nyumba pamoja na Post code ambazo zitarahisisha watu kufikiwa na huduma mbalimbali," alisema.

Waziri huyo alisema kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona duniani, biashara nyingi zilihamia mitandaoni lakini ni ngumu kufanikiwa kutokana na kukosekana kwa anwani za makazi.

"Biashara mitandaoni zinahitaji anwani za makazi za uhakika ili kuwafikia wateja, hivyo sisi kama serikali hatuna budi kuhakikisha mpango huu wa usambazaji wa anwani za makazi unafanikiwa ili wananchi kunufaika nao," alisema. Aliwataka wakuu hao wa mikoa kuhakikisha wanawashirikisha wananchi wote katika mpango huo wa usambazaji wa mfumo wa anwani za makazi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alisema maeneo mengi nchini bado ni vigumu kufikika kwa sasa kutokana na ukosefu wa mifumo ya anwani za makazi.

"Miji yetu inakabiliwa na uharifu mbalimbali kutokana na kutofikika. ni ngumu sana kufika katika maeneo mengi kutokana na kutokuwapo kwa anwani za makazi angalau hata kule kwetu Tanga kuna barabara ya kwanza hadi ya 22 lakini bado nyumba hazina namba," alisema.

Ummy alisema TAMISEMI kupitia wakuu wa mikoa watashiriki kikamilifu katika mpango huo wa usambazaji wa mfumo wa anwani za makazi kama ulivyokusudiwa.

RIPOTI MAALUM

# Mwanadada 'alivyotoka' kupitia kilimo mseto

## ■Avuna mamilioni kila nusu mwaka

**Na Mwandishi Wetu,** KOROGWE

KWA umri, jinsi, elimu na kazi yake ni nadra kukuta anajihusha na kilimo mseto, lakini akiwa na umri wa miaka 21 mwaka 2016, Monica Mizambwa alijikuta akivutiwa na kilimo mseto, akichanganya mahindi na maharage kwenye shamba la mkonge.

Monica, mama wa mtoto mmoja mwenye umri wa miaka minne, amekuwa mfano wa kuigwa wilayani Korogwe mkoani Tanga kwa kujikita kwenye kilimo hicho ambacho kimemwezesha kumudu maisha yake, pia kuendesha biashara.

Kijana Monica (26), ambaye ni Ofisa Kilimo wa Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) wilayani Korogwe, mbali na shughuli zake za ajira, amewekeza katika sekta hiyo ya taaluma yake, akiwa na shamba la mkonge lenye ukubwa wa hekta nne.

Mwanamama huyo kijana anayedokeza ana miaka miwili tangu aanze kuonja matunda ya jasho lake, ana simulizi ya ubunifu wa kipekee namna anavyochanganya mazao kuusindikiza mkonge ndani ya hekta hizo.

Kwa mujibu wa Monica, kwenye shamba hilo lililoko Kitongoji cha Mkokola, Kijiji cha Mkokola, Kata ya Magunga wilayani Korogwe, huwa anatumia ubunifu wa kunufaika na nafasi ya ardhi ulikopandwa mkonge kwa kadri anavyoweza.

Anataja matunda yake kwamba mbali na mkonge, eneo hilo linamnufaisha kwa mavuno ya mahindi, maharage na mimea jamii ya kunde.

Namna ubunifu huo unavyoendesha, mzaliwa huyo wa Chalinze mkoani Pwani anafafanua kitaalamu, akitamka:

"Unapofanya kilimo mseto kwenye mashamba ya mkonge, unakuwa unaitumia ardhi ipasavyo kwa sababu nafasi za kupanda mkonge kutoka mraba mmoja hadi mwingine ni mita nne.

"Sasa hiyo nafasi kubwa ya katikati unaitumia kupanda mazao ya msimu kama mahindi, maharagwe au mimea jamii ya kunde.



Sehemu ya shamba la kilimo mseto linalomilikiwa na Monica.

"Kwa hiyo, kuliko kuiacha hiyo ardhi ikiwa wazi, unaitumia kupanda mazao mengine ya msimu huku ukisubiri ile miaka mitatu ya mkonge kuwa tayari kuanza kuvunwa.

"Maharagwe unavuna baada ya miezi miwili, mitatu, mahindi miezi mitatu. Ukipanda mazao ya muda mrefu ni hatari kwa sababu mizizi yake inaenda mbali.

"Mizizi ikienda mbali inakutana na mizizi ya mkonge ambayo pia inaenda mbali. Mizizi ya mazao hayo ikikutana huko ardhini, lazima mmea mmojawapo utaathirika.

"Pili, mkonge huwa hauhitaji kivuli, unahitaji jua muda mwingi. Kwa hiyo, ukipanda mazao ya muda mrefu, mfano michungwa na mikorosho, yanaweka kivuli ambacho hakihitajiki kwenye mkonge.

"Mkonge ukishapata kivuli, nyuzi zake zinakuwa nyepesi. Kumbuka kuwa mwisho wa siku kinachouzwa na mkulima wa mkonge ni nyuzi kwa kilo."

Monica mwenye stashahada ya kilimo, ana ufafanuzi zaidi kwamba klimo mseto kwenye mashamba ya mkonge hufanyika ndani ya kipindi cha miaka mitatu baada ya mkonge kupandwa.

"Inaruhusiwa kuchanganya mazao ya msimu tu (ya muda mfupi) kama vile mahindi, mimea jamii ya kunde na pamba, lakini ni muhimu kuzingatia kwamba uchanganyaji huo unapaswa kufanyika kwenye miaka mitatu ya mwanzo baada ya mkonge kupandwa," anasema.

### FAIDA ZA KILIMO MSETO

Kuhusu manufaa ya kilimo mseto, Monica anasema ubunifu huo unamsaidia mkulima kurutubisha ardhi hasa pale anapotumia mimea jamii ya kunde kwa kuwa inatoa madini chuma na rutuba muhimu kwa udongo.

"Pili; kilimo mseto kinamsaidia mkulima kupunguza palizi kwa sababu mimea jamii ya kunde hufunika ardhi na hivyo kuzuia uotaji wa magugu.

"Tatu; kilimo mseto humsaidia mkulima kuwa na uhakika wa chakula kwa mazao anayolima kwa kipindi cha miaka mitatu anayosubiri kuanza kuvuna mkonge.

"Nne; mkulima anakuwa anajitosheleza wakati wote wa kulima mazao ya muda mfupi na kukidhi mahitaji yake mengine. Kwa hiyo mkulima anakuwa na uhakika wa chakula na fedha, hivyo anakuwa na fedha ya kuhudumia shamba," anasema.

### SAFARI YA MAFANIKIO

Monica anayepaza sauti kwa vijana kuwekeza kwenye kilimo cha mkonge na mseto wake, anasema alianza kujishughulisha na kilimo hicho miaka mitano iliyopita baada ya kupata darasa kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

"Kilimo cha mkonge na mseto wa mahindi kinakupa uhakika wa kuvuna magunia 20 kwa hekta moja. Jamii ya maharagwe ni magunia kuanzia 25 hadi 30 kwa hekta moja.

"Kwa mkonge ambao uko kwenye usimamizi mzuri zaidi, hekta moja mkulima ana uhakika wa kupata kuanzia Sh. milioni mbili hadi milioni 2.5 kwa hekta baada ya makato yote.

"Ukumbuke mkonge unavunwa mara mbili kwa mwaka, kila baada ya miezi sita unavuna. Mimi kwa sasa ni shamba la hekta nne, yaani ekari 10. Nilianza kulima mkonge mwaka 2016, lakini sikuanza kwa kupanda kwenye hekta zote nne.

"Mwaka 2016 nilianza kwa kupanda hekta mbili, kwa maana ya ekari tano. Huu nimeshaanza kuvuna. Mavuno ya kwanza mwaka 2019 nilipata Sh. milioni 1.2 baada ya makato yote.

"Makato hayo ni zile gharama za uzalishaji, mfano kwenye kuvuna tunatumia watu, kuna gharama za kusafirisha kutoka shambani hadi kiwandani, gharama ya kiwanda kinachochakata na kuna gharama ya chama ya uendeshaji kwa sababu tunafanya kazi chini ya Ushirika ambao pia una tozo zake," anasema.

Monica anabainisha kuwa uzoefu wake kwamba mavuno ya kwanza ya mkonge huwa ni madogo kwa sababu unakuwa si mzuri kutoa singa nzito, pia mkonge huo wa mavuno ya kwanza unakuwa si mrefu.

"Kwenye mauzo ya mkonge kinachozingatiwa ni urefu wa singa, kiwango chake na rangi. Rangi yenye soko zuri ni cream (rangi ya maziwa) isiyokuwa na doa lolote lakini urefu wa nyuzi zake uwe kuanzia sentimeta 60.

"Kwenye 'cut' (mavuno) ya kwanza, mkonge hauwezi kufika urefu huo wa sentimeta 60. Hiki kiwango cha juu kinapatikana kwenye 'cut' ya pili ama ya tatu.

"Mwaka 2017 nilipanda hekta moja na mwaka jana nilimalizia kupanda ya mwisho. Ninaendelea kuvuna maana mkonge unavuna mara mbili kwa mwaka.

"Mkonge hauhitaji mvua nyingi, kuna wadudu walikuwa wanaleta usumbufu lakini TARI wametusaidia dawa za kuwakabili. Mwaka wa kwanza nilipochanganya mahindi, nilivuna magunia sita lakini sikutumia mbegu bora.

"Mwaka wa pili sikulima tena mahindi, Nikalima maharagwe, nikapata magunia manane. Mwaka 2019, nikachanganya mahindi kwa mbegu bora, nikapata magunia 15 ya mahindi. Mwaka jana sikulima tena mazao mengine na hata mwaka huu sijachanganya kwa sababu muda umenibana. Wakulima wengine wanaendelea na wanafanya vizuri sana.

"Mwaka huu katika 'cut' ya kwanza ya mwaka nimevuna hekta mbili za mkonge na nimepata faida ya Sh. milioni 2.13. Kwa kifupi, kwa sasa nina uhakika wa kukidhi mahitaji yangu ya kifamilia na nimefanya vitu vingi vya kimaendeleo. Ninawekeza kwenye biashara fedha hizo za mavuno ya mkonge na mseto wake.

Monica ambaye pia anajishughulisha na kilimo cha tangawizi, anabainisha kuwa aliajiriwa kuwa Ofisa Kilimo wa Korogwe AMCOS mwaka 2019 baada ya kujitolea kufanya kazi hiyo kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2016, akiwasaidia wakulima.



Monica akiwa katika shamba lake la mkonge wilayani Korogwe.

ITAENDELEA

HABARI KITAIFA

# Maktaba kunufaisha wanafunzi Mkuranga

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wanafunzi 400 katika Shule ya Sekondari Lukanga wilayani Mkuranga mkoani Pwani watanufaika na maktaba iliyoboreshwa na kuwekewa vifaa muhimu na hivyo kuwafanya kusoma katika mazingira mazuri zaidi na kuongeza ufaulu.

Ukarabati wa maktaba hiyo umefanywa na taasisi isiyo ya kiserikali ya READ Tanzania kwa msaada kutoka Songas na wadau wengine wa maendeleo kwa gharama za Sh. milioni 28.5.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano hayo iliyofanyika katika viwanja vya shule hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa READ Tanzania, Magdalena George, alisema lengo la msingi la shirika hilo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuwezesha utoaji wa elimu bora nchini ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunzia shuleni.

Magdalena alisema ukarabati wa maktaba hiyo utawawezesha wanafunzi wa shule hiyo kusoma katika mazingira mazuri jambo ambalo litasaidia pia kuboresha ufaulu kitaaluma.

"Pamoja na ukarabati wa jengo hilo tumetoa vitabu 1,175, vitabu vya hadithi 194, viti 25, meza tano, shelfu tatu, kompyuta tatu zenye meza zake na vifaa vingine vya kusaidia wanafunzi kusoma vizuri," alisema.

Alipongeza Songas, Globeleq na washirika wengine kwa msaada wao wa kifedha unaoendelea kuwezesha ukarabati wa maktaba za shule katika maeneo mbalimbali nchini.

Johnson Makaranga, mwakilishi kutoka ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, aliipongeza taasisi hiyo kwa kutoa msaada wake kusaidia ujifunzaji kwa wanafunzi.

"Tumefurahishwa sana na juhudi hizi, ukarabati huu utawasaidia wanafunzi wetu hapa kusoma kwa raha katika muda wao wa ziada lakini pia wakati wa vitendo na hivyo kufanya vizuri katika mitihani ya shule na ya kitaifa," alisema.

Nicodemus Chipakapaka, Meneja wa Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi wa Songas, alisema kampuni hiyo imekuwa ikitoa msaada kwa maeneo ambayo yana athari kwa jamii.

"Tumekuwa tukisaidia READ Tanzania kukarabati maktaba na programu nyingine za elimu, kwa hili tunatarajia watoto wetu watasoma katika mazingira mazuri na hivyo kuweza kufikia ndoto zao," alisema.

Broke Mwita, mkuu wa shule hiyo, alipongeza READ Tanzania na washirika wake kwa kukarabati maktaba shuleni hapo, jambo ambalo litachochea zaidi utamaduni wa kujisomea miongoni mwa wanafunzi.

"Pia tumepokea vitabu vikiwamo vya hadithi, hivi vitaingiza tabia ya usomaji wa vitabu miongoni mwa wanafunzi wetu na hivyo kuinua uwezo wao wa kufikiri na maarifa," alisema.

Aliwataka wanafunzi kutumia vyema maktaba hiyo na kutunza vitabu hivyo ili kuhakikisha vinawanufaisha wengine.

# Uharibifu misitu watishia usalama

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Hamad Hassan Chande, amesema uharibifu wa misitu nchini umekuwa mkubwa na hivyo kutishia usalama.

Akizungumza juzi jijini Mbeya katika uzinduzi wa mradi wa urejeshwaji endelevu wa mazingira na hifadhi ya bioanuai, Chande alisema utafiti umebainisha kila mwaka nchi hupoteza wastani wa takribani hekta 469,420 za misitu na kusababisha upotevu mkubwa wa bioanuai inayochangia hatari ya kutoweka kwa baadhi ya aina muhimu za jamii ya mimea na wanyama.

"Kama kasi ya uharibifu wa mazingira isipodhibitiwa, nchi yetu itakuwa katika hatari ya kugeuka jangwa.

Kwa mfano, tathmini iliyofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii imeonyesha hali ya uharibifu ikiendelea hivyo katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2033, uharibifu wa misitu utaigharimu serikali kiasi cha Sh. bilioni 167 za kurejesha mazingira katika hali yake.

Kiasi hiki kingeweza kufanya shughuli za kimaendeleo katika taifa letu kama tutatunza mazingira vizuri." alisema.

Chande alisema kuwa nchi inakadiriwa kuwa na hekta millioni 48.1 za misitu, sawa na wastani wa asilimia 51 ya eneo lote la nchi kavu ambayo ina manufaa makubwa katika hifadhi ya bionuai ikiwamo makazi ya viumbe hai na vyanzo vya maji, ambavyo husaidia kupunguza joto ukaa na zaidi husaidia kutunza ardhi na kuifanya kuwa na rutuba. "Serikali haitavumilia kuona ubadhilifu wa aina yoyote katika utekelezaji wa mradi huu na kwa Ofisi ya Makamu wa Rais itakuwa mstari wa mbele kuhakikisha thamani ya fedha inaendana na miradi itakayotekelezwa katika maeneo yetu," alisema.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, alibainisha kuwa mradi huo unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 11.2, sawa na Sh. bilioni 25.7.

Alisema lengo la mradi huo ni kuimarisha usimamizi wa pamoja wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibika ili kuleta ustawi wa mifumo ikolojia na jamii kwa ujumla na ni sehemu ya mradi mkubwa wa kidunia (The Global Groject) unaotekelezwa katika nchi 11 duniani ikiwamo Tanzania.

Maganga alishukuru GEF na Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) kwa kushirikiana na serikali kupata fedha za utekelezaji wa mradi huo na Shirika la IUCN kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais katika hatua zote za maandalizi ya mradi.



Sehemu ya wakuu wa mikoa walioshiriki semina kuhusu anwani za makazi, iliyoandaliwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tuzo ya ubora bidhaa kuzinduliwa

**Na Joseph Mwendapole**

TUZO za ubora kitaifa zinazolenga kukuza sekta ya biashara kupitia ubora wa bidhaa na huduma katika ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) inatarajiwa kuzinduliwa kesho jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu kuzinduliwa kwa tuzo hizo, Meneja Uthibiti Ubora wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Gervas Kais, alisema jukumu la kuandaa tuzo hizo limekabidhiwa kwa shirika hilo kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

"Tumekabidhiwa jukumu la kuanzisha Tuzo za Ubora za kitaifa na Wizara ya Viwanda na Biashara kufuatia makubaliano baina ya wananchama wa SADC ili kutambua na kukuza sekta ya biashara kupitia ubora wa bidhaa na huduma katika ukanda huu," alisema Kaisi.

Alifafanua kwamba tuzo hizo ni sehemu ya mipango ya serikali katika kuboresha huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini kupitia matumizi ya viwango na kanuni za ubora wa taasisi za umma na sekta binafsi ili kuhakikisha mifumo, bidhaa na huduma zinakidhi mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa, hivyo kufanya vizuri kwenye masoko ya ngazi zote hizo.

"Juhudi hizi ni uti wa mgogo wa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi hasa katika mapinduzi ya nane ya viwanda," alisema Kaisi na kuongeza kwamba juhudi hizo zitaleta hamasa kwa wazalishaji wa bidhaa na watoa huduma, hivyo kuongeza ushindani sawia.

Alisema mashindano hayo yatafanyika katika vipengele vitano ambavyo ni tuzo kwa kampuni bora ya mwaka, tuzo kwa bidhaa bora ya mwaka, tuzo kwa huduma bora ya mwaka, tuzo ya muuzaji bora wa bidhaa nje ya nchi na tuzo kwa mtu mmoja aliyefanya vizuri kwenye masuala ya ubora.

Alifafanua kwamba kwa kipengele cha kwanza hadi cha nne zimeandaliwa tuzo kwenye makundi mawili kwa kila kipengele, yaani tuzo kwa kampuni kubwa na tuzo kwa kampuni ndogo au wajasiriamali wadogo. Alisisitiza kwamba kipengele cha tano kinahusu mtu mmoja pekee.

Kwa mujibu wa Kaisi, hafla ya uzinduzi wa tuzo hizo kitaifa kwa mwaka 2021/22 itaambatana na kukamilika kwa utolewaji tuzo kwa washindi waliopatikana mwaka 2020 kupitia mashindano yaliyoandaliwa na TBS kwa kushirikiana na TPSF, SIDO, ZBS, TWCC, TUCTA na TaNTRADE.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maagizo kuhusu mafao, bima yatekelezwe hima

**WAZIRI** Mkuu Kassim majaliwa, juzi aliahirisha mkutano wa tano wa Bunge la 12 jijini Dodoma kwa kutoa maagizo mazito ambayo kwa muda mrefu yamekuwa kikwazo kwa makundi mbalimbali na hata kuonekana kwamba serikali haitekelezi ahadi zake au kutatua kero zinazowahusu.

Wakati wa mkutano huo katika baadhi ya mijadala, wabunge waliibua masuala ya mafao kwa wastaafu, bima ya afya kwa wote na kupanda ghafla kwa bei ya mbolea. Kwa ujumla, mambo hayo yalitikisa mkutano huo kiasi cha Spika Job Ndugai kutoa maagizo kwa serikali kuwasilisha majibu ya kero hizo na utekelezaji wake.

Kutokana na hoja hizo kutikisa, Waziri Mkuu Majaliwa kwa niaba ya serikali, aliagiza kutatuliwa haraka tatizo la ucheleweshaji wa mafao ya wastaafu katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Katika kutekeleza hilo, Majaliwa, alimtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Uratibu na Watu Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, kushirikiana na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuhakikisha vikwazo katika upatikanaji wa mafao ya wastaafu kwa wakati vinaondoka.

Aliweka bayana kwamba hakuna haja ya mstaafu kuanza kuhangaikia mafao yake baada ya ajira kukoma na badala yake alipwe mara moja stahiki yake mara anapostaafu.

Sambamba na mafao, serikali pia iliiagiza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuandaa na kuwasilisha bungeni muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili kutungiwa sheria na kuhakikisha kuanzia mwaka ujao wa fedha ianze kutumika .

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, suala hilo linapaswa kufanyiwa kazi haraka ili kuhakikisha linaanza kutekelezwa mwaka wa fedha wa 2022/23 ili kila mwananchi awe na uhakika wa kupata matibabu kila inapolazimu. Alisema sheria hiyo inapaswa kupatikana haraka ili kutimiza malengo na ahadi ya serikali kuhusu upatikanaji wa huduma za afya kwa gharama nafuu hasa kwa kutumia mfumo wa bima ya afya.

Masuala hayo mawili, yaani bima ya afya kwa wote na mafao kwa wastaafu, yamekuwa kero kubwa kwa wahusika na wananchi kwa ujumla kutokana na kusuasua kwake. Kwa mantiki hiyo, agizo la Waziri Mkuu linatoa matumaini kwamba yatafanyiwa kazi na wahusika kwa kasi kubwa.


Mafao kwa wastaafu kwa mfano, ni tatizo ambalo limekuwa sawa na donda ndugu na mateso kwa wahusika. Limekuwa jambo la kawaida kuona kwamba mtumishi ambaye amelitumikia taifa kwa takribani miaka 40, anaona utumishi wake ni majuto badala ya fahari kutokana na kuhangaikia mafao ambayo sehemu amekuwa akikatwa kutoka katika mshahara wake.

Baadhi ya wastaafu wamekuwa wakikumbana na vikwazo mbalimbali katika kupata haki zao hizo kutokana na kufuatilia mafao hata miaka mitano au zaidi. Hata wanapofika katika ofisi husika hupewa majibu ya kukatishwa tamaa kama vile taarifa kutokupatikana na wakati mwingine kujengewa mazingira ya kutoa rushwa. Hatua hiyo imesababisha baadhi ya wastaafu kupoteza maisha wakiwa hawajafaidi matunda ya utumishi wao.

Kwa upande wa bima ya afya, ni dhahiri kwamba asilimia kubwa ya Watanzania hawana uwezo wa kugharimia matibabu yao na ya wategemezi wao kwa kutumia fedha zao za mfukoni. Kwa serikali kuagiza kuharakishwa kwa sheria hiyo, kunatoa faraja kwamba Watanzania wengi watapata ahueni ya kupata huduma za afya kwa urahisi kupitia bima ya afya.

Hata hivyo, ni rai yetu kwamba maagizo hayo yatatekelewa na wahusika kama ilivyoagizwa na serikali kwa kuwa kuna mambo mengi yametolewa maagizo na maazimio lakini hayajatekelezwa na matokeo yake wananchi kuona kuwa vinavyofanyika ni siasa za kuwapaka watu mafuta kwa mgongo wa chupa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ubovu mabomba udhibitiwe kukabili makali mgawo maji

**MAMLAKA** ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imetangaza mgawo wa maji, katika Mkoa wa Dar es Salaam kutokana na kile ambacho inaeleza kuwa ni upungufu wa maji katika Mto Ruvu.

Pamoja na kutangaza hali hiyo, kuna maeneo hayataathirika na mgawo huo ambayo ni Kisarawe, Chalinze, Pugu, Bagamoyo, Oysterbay, Masaki, Mikocheni, Ikulu, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Kikwete (JKCI) na Soko Kuu Kariakoo.

Upungufu wa maji katika mto huo, unasababisha mamlaka hiyo kuandaa utaratibu wa kuhakikisha hakuna mwananchi ambaye atakumbana na kero ya ukosefu wa maji kutokana na kiangazi cha muda mrefu.

Katika utaratibu huo, DAWASA inasema imejipanga kuhakikisha vibali vya watumiaji wengine ikiwa ni pamoja na vya wakulima vinasitishwa huku shughuli za kunywesha mifugo katika mto pia zimesitishwa.

Pamoja na hayo, mamlaka hiyo inasema, mto huo kwa majuma mawili bado iko palepale ambapo kina cha maji kiko katika mita 1.5 hadi 1.8, huku Ruvu Juu kina kikiwa mita 16 hadi 18 hivyo hali ya mito kuendelea kuimarika.

Nimejaribu kueleza kwa kifupi kile ambacho mamlaka hiyo inakifanya ili kuhakikisha wananchi wanapata unafuu katika kupata huduma hiyo muhimu wakati huu ambao mgawo wa maji umetangazwa.

Lengo langu ni kutaka kukumbusha DAWASA na wananchi kwa ujumla umuhimu wa kujali miundombinu ya maji kutokana na umuhimu wa huduma hiyo katika maisha ya kila siku.

Imekuwa ni kawaida kukuta mabomba ya maji yamepasuka na kuachwa kwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo, hali ambayo inasababisha maji mengi kupotea ardhini huku baadhi ya watu wakikosa huduma hiyo.

Inawezekana chanzo cha mabomba kupasuka na kuachwa kwa muda mrefu bila kutengenezwa ni wananchi wenyewe kutotoa taarifa kwa mamlaka husika au ni mafundi kuchelewa kuchukua hatua.

> **Imekuwa ni kawaida kukuta mabomba ya maji yamepasuka na kuachwa kwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo, hali ambayo inasababisha maji mengi kupotea ardhini huku baadhi ya watu wakikosa huduma hiyo.**

Wakati huu ambao mgawo wa maji, ingefaa kila upande kuwa makini mara tu unapotokea uharibifu, taarifa zifike haraka kwenye mamlaka husika na pia mafundi wawe wepesi kwenye eneo la tukio.

Hayo yakifanyika, itakuwa rahisi kuzuia maji yasipotee, lakini wananchi wakikaa kimya na kudhani si wajibu wao kutoa taarifa za uharibifu au ubovu wa miundombinu ya maji, wanaweza kuchangia ukubwa wa mgawo.

Mafundi nao kwa upande wao wakipewa taarifa wakachukua wiki au zaidi ya hapo bila kufika kwenye tukio, watakuwa wanachangia kuwapo kwa upotevu wa maji na ongezeko la mgawo.

Hivyo njia nzuri ni kila upande kutimiza wajibu, kwa ajili ya kuzuia upotevu wa maji usio wa lazima ambao wakati mwingine unaweza kuwa unasababishwa na uzembe wa wananchi au mafundi wa DAWASA.

Ninatambua juhudi zinazochukuliwa na DAWASA kuhakikisha huduma ya maji inaboreshwa ikiwa ni pamoja na kuhamisha maji kutoka katika vyanzo vyake vingine ili kuhudumia maeneo ambayo hakuna huduma hiyo.

Kwa mfano mtambo wa Ruvu Juu, imetumika kuhudumia maeneo ambayo awali yalikuwa yakipata huduma hiyo kutoka katika mtambo wa Ruvu Chini lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na uhakika wa kupata maji.

Lakini pia vyanzo vyake vingine vya mtambo wa mtoni pamoja na visima virefu vinaendelea kutoa huduma katika maeneo mengine ya jiji ili kupunguza uhaba wa maji uliopo Jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, juhudi hizo zinaweza zisizae matunda iwapo miundombinu ya kusafirisha maji kwenda kwa watumiaji itaendelea kuharibika na kuchukua muda mrefu bila kukarabatiwa kama ilivyo sasa katika baadhi ya maeneo.

## SAFU

### KWA MASLAHI YA TAIFA

# Hongera TotalEnergies kwa kujengea uwezo Watanzania



Na Pascal Mayalla

BABA wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema: “Umaskini mbaya kabisa, ni umaskini wa fikra” au umaskini wa mawazo. Hiyo inatokana na ukweli kwamba Watanzania wengi wanaishi katika umaskini uliopotea.

Umaskini huo unaendelezwa kwa maskini hawa kuwa na fikra za kimaskini, kuwa na mawazo ya kimaskini na matokeo yake wanaendelea kubaki maskini daima na kizungumkuti cha umaskini (vicious circle of poverty).

Licha ya taifa letu kuingia kwenye uchumi wa kati, ukweli unabaki pale pale kwamba kati ya Watanzania walala heri na walala hoi, walala hoi ni wengi zaidi. Kadri siku zinavyokwenda ule msemo wa mwenye nacho anaongezewa na asiye nacho, ananyang’anywa hata hicho kidogo alicho nacho, ndivyo Watanzania wasio nacho wanazidi kuwa masikini. Wenye nacho ndio wanaongezewa na ndio wanaofaidi uchumi huu wa kati.

Japo takwimu zinaonyesha kukua kwa uchumi kwa kasi ya asilimia saba, sekta zinazochangia ukuaji huo si zile zenye watu wengi. Sekta ya kilimo inayoongoza kwa kuajiri watu wengi, ukuaji wake ni chini ya asilimia tatu.

Kwa mantiki hiyo, asilimia 67 ya wanaotegemea kilimo cha kujikimu ni wakulima masikini.

Hivi karibuni, Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, alisema kati ya Watanzania milioni 60, Tanzania ina mabilionea 5,000 tu sawa na asilimia 0.008 ya Watanzania na wanamiliki asilimia 4.2 ya utajiri wote katika kundi la mabilionea wa Afrika.

Katika mabilionea hao 5,000 wa Tanzania, 100 wanamiliki zaidi ya asilimia 28 ya utajiri wote wa mabilionea wanaotoka Tanzania.

Ili mtu kuwa bilionea, si lazima uwe na mapesa zaidi ya bilioni moja kwenye akauti yako. Unaweza kuwa na rasilimali zenye thamani ya zaidi ya bilioni moja, ukawa bilionea.

Lakini kwenye hesabu za mabilionea hao, unaweza kuwa haupo kwa sababu idadi hiyo imepatikana kwa mabilionea rasmi tu, wenye nambari ya TIN na wanalipa kodi.

Wakati Betty Mkwasa akiwa DC wa Bahi, kuna Msukuma mmoja anamiliki zaidi ya ng’ombe 5,000 huku akiwa na zaidi ya wake 20, watoto 60 na wote wako kwenye boma lake.

Huwezi kuamini hao ng’ombe thamani yake ni zaidi ya Sh. bilioni lakini mtu huyo alikuwa anaishi kwenye nyumba ya nyasi, anatembea kwa miguu!

Kupitia mbio za Mwenye, akashauriwa kuuza baadhi ya ng’ombe akanunua bati, akajenga nyumba za kisasa, akashauriwa kujenga shule ya watoto wake na serikali imempelekea walimu.

Sasa ana magari, pikipiki na baiskeli. Tanzania tuna mabilionea wengi wa hivi ambao ni matajiri wa mali lakini masikini wa fikra.

Kutokana na umaskini huu, kuna nchi wafadhili, marafiki na washirika wa maendeleo, wanatuletea miradi mbalimbali ya misaada ya ufadhili.

Wengine wanatuletea hata chakula wakati wa njaa. Kuna wafadhili wa nchi fulani walituletea samaki vibua, kisha wakaleta meli yao kuvua samaki wetu na kutupatia samaki tule badala ya kutufundisha kuvua samaki ili tujitegemee.

Hivi ndivyo hali ilivyo kwa baadhi ya mashirika na kampuni zinazofanya biashara Tanzania.

Kampuni hizo zina mipango ya kurudisha kile kidogo kwa jamii. Mara nyingi hugawa chakula au misaada kwa wahitaji.

Lakini kampuni ya mafuta ya TotalEnergies, licha ya kutoa misaada mbalimbali kwa jamii, imejitolea kuzalisha mabilionea wa Kitanzania wenye wazo zuri la biashara. Kupitia mpango huo, wanatoa zawadi hadi Sh. milioni 20 na washindi watatu wa shindano hilo wanaingia kwatika shindano kubwa la Afrika.

Hivi sasa ni awamu ya tatu ya shindano hilo, maarufu kama ‘Start Uper of the Year Challenge by TotalEnergies’ kwa mwaka 2021 - 2022. Hilo ni shindano la kitaifa lenye lengo la kutambua, kuwazawadia na kuwawezesha wajasiriamali wachanga ambao wameanzisha biashara zisizozidi miaka mitatu na zenye matokea chanya kwa jamii.

Kutokana na mafanikio makubwa ya awamu mbili za awali ambazo zilifanikisha kuwezesha wajasiriamali vijana kama Doreen Noni, Michael Sayi na Prince Tillya ambao walikuwa washindi wa mwaka 2019, sasa ni awamu ya tatu kutafuta mabilionea wengine wapya.

Hii ni uthibitisho wa nia ya TotalEnergies kusaidia maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini kwa kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana.

Shindano litawawezesha kifedha na mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 35 ambao wanaendesha miradi ya kibiashara katika sekta yoyote ya uchumi.

Washindi watatu watachanguliwa kwa kuzingatia mradi bora unaowezesha kuanzisha biashara nyingine; biashara bora isiyozidi miaka mitatu; na mjasiriamali bora wa kike.

Kila mshindi atajinyakulia kitita cha Sh. milioni 20 na watapata fursa ya kutangaziwa biashara zao na Total Energies pamoja na mafunzo ya ziada ya ujasiriamali kulingana na ubunifu wa mradi wa biashara zao.

Zaidi ya hayo, washindi hao wataandikishwa kwenye shindano la Startupper Challenge kwa bara la Afrika ili kupata washindi watatu wakuu kwenye bara zima.

Lengo la TotalEnergies ni kuongeza kasi ya suluhisho la tatizo la ajira kwa vijana barani Afrika. Ingawa shindano hili halitatatua kikamilifu, litajenga mawazo ya kibunifu na kusaidia vijana wajasiriamali wenye ari.

Ni wakati sasa kwa wazazi kuwahamasisha vijana wajasiriamali kuchukua fursa hii iliyofunguliwa Novemba 4 na pazia litafungwa Desemba 23. Kinachofanywa na TotalEnegies kifanywe na kampuni zingine ili kuondokana na utegemezi kutoka kwa wafadhili.

**0754270403**
**pascomayalla@gmail.com**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Wenye mabasi ya mwendo kasi jiongezeni



Na Joseph Kulangwa

**Mimi hii kauli ya Chifu Hangaya iliningia kisawasawa kwani ina busara kwa sababu hivi unamlazimishaje punda kunywa maji wakati hana kiu? Mtu kazoea kulalia kirago leo unambwagia godoro sijui la Dodoma, atalilalia kweli? Mwache kazoea kugalagala chini huyo.**

JUZI kati hapa, Chifu Hangaya alitoa tamko fulani zito lakini naona kama watu walilichukulia kirahisi tu bila hata kutulia na kulitia maanani kuwa limetoka kwa Mkuu wa Nchi.

Kama mmesahau nakukumbusheni, Chifu alisema haya masoko haya, tuliyoyabadilisha na kuyajenga kisasa, kuyajenga maghorofa haya, lakini walengwa wakaonekana kuyasusa, tuyafanyie kazi.

Akasema kama wajasiriamali hawa wanaona ni nongwa kuuzia vitu vyao kwenye maghorofa na badala yake wanaona heri kutandaza chini, basi watafutiwe kwingine kwenye mavumbi wanakotaka.

Lakini haya maghorofa ambayo yametafuna vijifedha vyetu, basi yageuzwe kuwa kumbi za harusi ili yasikae kimagofugofu au kimapagalapagala na kuoza tu na kuwa makazi ya popo, buibui, nyuki na manyigu.

Akasema Chifu Hangaya ili yasikae bila kuzalisha basi yakigeuzwa kumbi za harusi chochote kitu kitapatikana kwa maendeleo ya nchi yetu. Kama mmekumbuka, sasa mnasemaje?

Uzuri wa Wabongo wakishasikia hivyo, utawaona siku ya kwanza, ya pili, ya tatu wanachakarika, baadaye wanasahau tena maisha yanaendelea kama kawaida! Ukibisha angalia ni nani sasa hivi anavaa barakoa!

Mimi hii kauli ya Chifu Hangaya iliniingia kisawasawa kwani ina busara kwa sababu hivi unamlazimishaje punda kunywa maji wakati hana kiu? Mtu kazoea kulalia kirago leo unambwagia godoro sijui la Dodoma, atalilalia kweli? Mwache kazoea kugalagala chini huyo.

Kauli hii inaendelea kugonga kichwani mwangu ninapoona maghorofa yaliyotelekezwa Dar es Salaam, baada ya watu kuhamia Dodoma. Leo ni kama mahame yanakaliwa na mbu, popo na buibui.

Unajiuliza sasa haya yatafanyiwa nini? Unashangaa, yageuzwe shule? Nani atasoma humo na atasomea nini? Yageuzwe hospitali? Nani atatibiwa humo kwa ugonjwa gani? Basi tunabaki kushangaa tu na kujiuliza nini kifanyike.

Wakati hilo halijanitoka kichwani, napita kandokando ya barabara hizi za mabasi wanayoyesma yanakwenda haraka. Naangalia mabanda haya ambamo abiria wanatakiwa kuyasubiri.

Sehemu nyingi ninamopita, sioni abiria wa kuyajaza yale, lakini pia sioni mabasi mengi kuegesha kwa wakati mmoja! Najikuta najiuliza tena hapa, hivi waliyoyajenga haya kwa urefu huu wa karibu meta 100 walimaanisha nini?

Kwa wenzetu wa Ughaibuni ambako ni hakika ndiko tulikoona na kuiga, mabasi kama haya unaweza yakuta kituoni yakiwa zaidi ya matano na kuondoka kwa kupishana sekunde tu, hivyo eneo hilo kusheheni mabasi.

Tofauti na hapa kwetu, basi linaweza kukaa hata dakika tano au kumi kusubiri abiria utadhani si la kwenda haraka, linakuwa sawa na daladala lingine tu la Massawe. Hivyo utakuta mabanda hayo yako wazi kabisa muda mwingi.

Sasa hukaa na kujiuliza, hivi kwa nini kusiwapo na namna mbadala ya kutumia kikamilifu vituo hivyo, ambavyo sehemu kubwa hubaki kumbi za wazi, huku sehemu ndogo tu ikitumika kwa abiria ambao hata hivyo muda wote husimama na si kukaa.

Kwa nini wamiliki wa kampuni hiyo ya mabasi yaendayo haraka wasibuni hata kuanzisha vijimigahawa katika maeneo yaliyo wazi, ili abiria anayesubiri basi, awe anapata kitu chai au kahawa na vitafunwa vingine, kabla ya kuendelea na safari?

Hivi mnashindwa kujiongeza mkafikiria kuwa kwa wengine kufika kwenye vituo hivyo na kupanda mabasi ya mwendokasi ni mtoko? Mnashangaa nini wakati mnaona kila siku watu wamejipanga daraja la Manzese kupiga picha?

Nendeni Dodoma mwone Nyerere Square watu wanavyojikusanya pale kupiga picha za kumbukumbu kwamba nilifika pale. Kwani hamwoni kuwa watu wanakuja Dar es Salaam kupiga picha kwenye mwendokasi na kutuma kwao?

Kama wahusika hamlijui hilo, basi jishughulisheni kidogo kwa kwenda hata kwenye madaraja ya Kijazi, Mfugale, Buguruni na hata lile la Nyerere Kigamboni na sasa linakuja la Tanzanite, mjionee mitoko.

Mkiweka vijimigahawa kwenye mastendi yenu ya mwendokasi au hata vijibaa tu, mtaona jinsi mtakavyoingiza fedha badala ya kutegemea nauli za kwenye mabasi. Jiongezeni, oneni majengo haya hayatumiki kikamilifu. Mpo?

**Alamsiki!**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Fedha za IMF zisinyanyapae wafanyabiashara



Na Thobias Mwanakatwe

**Nimeona mahali barua za viongozi wa serikali ya Mkoa wa Mbeya ikiwamo ya Halmashauri ya Wilaya Mbeya wakitoa maelekezo ya kutaka fedha zilizoenda kwenye akaunti za shule kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kurejeshwa katika akaunti za halmashauri kisha kwenda akaunti ya Katibu Tawala wa Mikoa (RAS).**

OKTOBA, mwaka huu, serikali ya Tanzania ilipata mkopo wa Sh. trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Dunia (IMF).

Baada ya kupata fedha hizo, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kupitia kwa waziri wake, Ummy Mwalimu, ilisema kati ya fedha hizo, wizara yake imeidhinishiwa Sh. bilioni 535.6 sawa na asilimia 41.1 ya fedha zote.

Ummy alisema Sh. bilioni 302.7 zitatumika katika sekta ya elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa 12,000 vya sekondari ili kuwezesha wanafunzi wote kuanza masomo kwa wakati mmoja.

Kutokana na mgawo huo, alitoa maelekezo kuwa katika utekelezaji wa miradi hiyo Halmashauri zinaweza kutumia makandarasi wa ndani au utaratibu wa "force account".

Pia aliwaelekeza wakurugenzi wa halmashauri zote nchini waendelee na ujenzi wa madarasa hususani kwa shule za msingi na kukamilisha ununuzi wa viti, meza na madawati katika vyumba vya madarasa ya zamani ili kujenga mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji.

Pamoja na maelekezo hayo ya waziri kuhusu fedha hizo, kilichoanza kufanywa na serikali ya Mkoa wa Mbeya, hakikubaliki na huku ni kuleta ubaguzi usio na tija kwa wafanyabiashara.

Nimeona mahali barua za viongozi wa serikali ya Mkoa wa Mbeya ikiwamo ya Halmashauri ya Wilaya Mbeya wakitoa maelekezo ya kutaka fedha zilizoenda kwenye akaunti za shule kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kurejeshwa katika akaunti za halmashauri kisha kwenda akaunti ya Katibu Tawala wa Mikoa (RAS).

Fedha ambazo zimeombwa kurejeshwa ni zile za ununuzi wa mabati na saruji ili eti mkoa ukanunue kiwandani badala ya kwa wafanyabiashara ambao ndio hao hao wanaowategemea kulipa kodi.

Kutonunua saruji na mabati kwa wafanyabiashara hawa maana yake hatutaki mzunguko wa fedha uwaendee watu wengi zaidi mtaani ambako vyuma vilikaza.

Pia ziko barua za maelekezo kutoka kwa wakurugenzi kwenda kwa maofisa elimu msingi na serikali zikiwaelekeza kuzirejesha fedha hizo kwenye akaunti ambazo zimeorodheshwa kwenye barua hizo.

Binafsi sioni msingi wa ushauri huo ukizingatiwa kuwa wakati Mbeya ni sehemu ambayo ujenzi gharama yake ipo chini.

Kwa mikoa ambayo ujenzi wake uko chini ukiwamo Mbeya, hawakupaswa kufuata ushauri ambao ulilenga maeneo ambayo kuna gharama kubwa za ujenzi.

Tukirejea maelekezo ya fedha hizo kutoka kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, alisema kuwa fedha hizo zinakwenda kusisimua hata mzunguko wa fedha mitaani.

Kuna diwani mmoja katika Mkoa wa Songwe amesema amekataa fedha hizo kurejeshwa mkoani na wakitaka wazichukue zote.

Katika wachangiaji wa suala hili, mmoja wao anasema hili la mkoa kufanya ununuzi ya pamoja ya saruji, hapana hata kama wana nia nzuri lakini yawezekana hawajaelewa 'essence' ya huu mkopo.

Lengo kuu la mkopo huu ni kusisimua sekta mbalimbali zilizoathiriwa na janga la corona.

Ukifanya ununuzi wa pamoja unamwondoa kwenye mnyororo wa saruji muuzaji wa kawaida ambaye kupitia yeye angeweza kuleta huo msisimko kwa mtu wa kawaida kabisa na bado wazalishaji wakanufaika.

Pili, unapofanya hivyo moja kwa moja kiwandani pale Mbeya Cement, ina maana unapeleka hizi fedha nje kwa kuwa anayemiliki hisa kubwa zaidi pale ni kampuni ya nje.

Wakuu wa shule waachwe wafanye ununuzi sehemu ambako huwa wanakopa wanapotekeleza miradi ya ujenzi. Hii itasaidia hii fedha kubaki ndani ya maeneo husika miradi inapotekelezwa.

Uamuzi huu wa mikoa kuzitaka fedha hizo zirejeshwe halmashauri ili ununuzi ufanyike kiwandani ni kama urafiki wa ng'ombe na viboko.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**
**mwanakatwe2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# MADHARA YA UMBEA NA MAJUNGU KATIKA FAMILIA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Wakati mwingine ulimi umetumika kusema uongo na kuchafua mtu au watu kwa lengo la kuharibu. Mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari wakati mwingine vimetumika kusambaza habari za uongo na kuchafua watu.**

TUNAISHI katika jamii ambapo ubinadamu unatawala hali ya ki-Mungu ndani ya binadamu. Watu wengi wamejeruhi wenzao kwa sababu ya umbea na majungu. Katika kipindi hiki ambapo tunapambana na adui korona, manyanyaso, dhuluma, ukatili wa kijinsia na maadui wengine, hatunabudi kupambana na adui umbea na majungu, kwani mambo haya yamewajeruhi, kuvuruga watu na kusababisha vifo katika jamii.

Wakati umefika kila mmoja wetu kutafakari na kujiuliza pasipo aibu na kujihurumia ni kwa jinsi gani ametumia silaha ya umbea na majungu kujeruhi watu wengine.

Umbea na majungu ni dhambi kama dhambi zingine. Umbea na majungu ni uovu, ubinafsi, aina ya ugaidi, upagani; ni kupoteza imani na upendo kwetu na kwa watu wengine. Umbea na majungu ni dhambi kubwa kwa sababu huwajeruhi watu wengi, huharibu heshima na sifa za watu, huvunja uhusiano baina ya watu na marafiki, na kusambaratisha familia na jamii.

Umbea huzungumzwa kirahisi, husikilizwa kwa makini na kusambazwa kwa haraka sana. Mbaya zaidi watu wengi huamini mambo ya umbea kuliko wanavyoweza kuamini mausia na mafundisho yenye kujenga.

Ugaidi wa umbea na majungu msingi wake ni ulimi. Wakati mwingine ulimi umetumika kusema uongo na kuchafua mtu au watu kwa lengo la kuharibu. Mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari wakati mwingine vimetumika kusambaza habari za uongo na kuchafua watu. Mtu mmoja anapochafuliwa, hali hiyo haimhusu yeye tu bali familia yake, wazazi wake, ndugu zake na watu wengine wanaomtegemea. Mtu mmbea na mpiga majungu ni gaidi anayewaangamiza watu wengine.

Umbea na majungu, wivu, husuda na chuki hujibainisha katika kutothamini kazi nzuri za wenzetu, kupinga sifa zitolewazo kwa mema waliyotenda ili kuhalalisha uzushi na kumdhalilisha mtu mwengine.

Katika jamii tunayoishi wako watu ambao kazi yao ni kufitinisha watu wengine kwa kutafuta na kusafirisha habari.

Watu wa aina hii hupenda kusikia mambo ya wengine na kuyapeleka kwa wengine. Hali hii huvuruga amani na mshikamano katika familia na jamii. Umbeya na majungu ni dalili ya kufilisika kifikra na kimawazo. Umbeya na majungu ni hatari kwa amani na mshikamano katika familia na jamii kwani huchochea vurugu, fujo, mpasuko wa kifamilia na kijamii.

Kila mtu ajifunze kuwafikiria na kuwanenea watu wengine mema, kwani wema na ubaya ni akiba. watu wasiendekeze umbea na majungu dhidi ya wale ambao hawawapendi au hawaelewani nao au wanaojisikia kuwa wanyonge kwao.

Ni vizuri na ucha Mungu kukabiliana na mtu uso kwa uso au ikibidi tumia mtu mwingine mwenye hekima kutafuta suluhu kadri ya busara na hekima itokanayo na upendo. Waheshimu watu wengine. Usiwatendee wengine yale ambayo wewe hupendi kutendewa nao. Apandaye mbegu ya fitina, atavuna zao la fitina yake.

Ndugu msomaji wa makala hii, usiseme jambo kuhusu mtu mwingine, kwa kile ambacho huna ujasiri wa kusema na mpiga huyo akiwa mbele yako. Wanenee wengine yale upendayo wakusee wewe.

Unaposikia mambo ya umbea, usiyafurahie wala kuyachangamkia ili usishiriki dhambi hiyo.Mbea na mpiga majungu anapoanza kusema mambo yake mkanye, muelemishe au badili mazungumzo au onesha kutokujali.

Jenga ukuta mkubwa masikioni mwako dhidi ya umbea, majungu na uzushi. Busara na hekima ya maisha inatudai kuzuia midomo yetu, kutawala ndimi zetu na kuepuka fitina. Kumbuka wakati wote kuwa, anayekueleza mambo ya wengine akifika kwao ataongea mambo yako pia. Umbea na majungu imekuwa silaha ya watu waoga na dhaifu ambao hawathubutu kukabiliana na watu ambao wanahisi kutokuelewana nao au waliowazidi uwezo.

Umbea na majungu ni kichaka na maficho ya watu wavivu katika wajibu na kazi.

Watu wa aina hii hawana muda wa kuchosha akili zao kufikiri na kubuni mambo yenye tija. Hivyo, dhamiri zao zinawasuta wanapoona wengine wakifanikiwa au kusifiwa kwa kazi njema.

Uhusiano mbaya baina ya dunia na wakaaji wake, baina ya Mungu na watu wake, baina ya ndugu na ndugu, waumini kwa waumini na watumishi kwa watumishi, ni matokeo ya tamaa ya vitu, hali, hadhi na heshima ambayo inaibua na kuchochea hali ya wivu, chuki na husuda inayojieleza na kujipambanua katika umbea na majungu. Umbea na majungu ni mtaji wa watu dhaifu na wasiojitambua.

Viongozi katika ngazi ya familia na jamii wanaalikwa kuwa sehemu ya suluhu na si tatizo. Viongozi tunapaswa kuwa sababu ya kuleta uponyaji katika dunia dhidi ya hali hii ya ugaidi wa umbea, majungu, uzushi na fitina. Viongozi wana wajibu wa kujenga uhusiano bora baina ya muumba na viumbe, baina ya watu na viumbe.

Pia viongozi kujiingiza katika umbea na majungu ni kujikosea na kuwakosea wanaowaongoza. Viongozi wanapaswa kuwa wapatanishi na watafuta maridhiano na suluhu juu ya changamoto. Mungu akusaidie kutoka kwenye uhaini wa umbea na majungu kwani si dili. Kumbatia upendo, utu wema na fadhili na utayari wa kutenda mema kwa binadamu mwingine ili Mungu akutakabali.

**●Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**


# MAISHA

NOVEMBA 14, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




Ukurasa 13

**Mtindo wa kofia unaoshangaza**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Namna ya kuchagua muundo wa ngazi ndani ya nyumba





## HARUSI


Ukurasa 12



# Wacha midomo iseme

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




| | |
|---|---|
| KITABU | PENI |
| BARUA | BAHASHA |
| FUNGUO | KUFULI |
| BEKI | MPIRA |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | B | O | M | B | A |
| | A | | | E | |
| O | N | A | | M | |
| | A | | I | B | A |
| | N | | | E | |
| P | A | M | B | A | |

## AMSHA AKILI





## TOA TOFAUTI 5




## WATOTO

# PAKA RANGI





## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
DUA, MWA, BAINI, UHURU, RASULI, UTWANA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Shabani alikuwa akisikiliza hadithi kutoka kwa bibi yake, siku hiyo bibi yake alikuwa akimsimulia hadithi za kale ambazo zilimfanya kuwa na udadisi mwingi. Mwishoni bibi yake alimalizia simulizi yake kwa kumwambia kuwa 'asiyesikia la mkuu huvunjika guu'.

**Shabani:** Bibi nimekuelewa na mimi kuanzia leo nitasikia ya wakubwa.

**Bibi:** sawa mjukuu wangu usije yakakufika makubwa kama yaliyo kwenye hadithi.

**Shabani:** Naogopa kwani naweza nikavunjika miguu yangu, kama ulivyosema mwisho.

**Bibi:** (akacheka) Hapana sio kuvunjika miguu bali usiposikia kwa watu waliokuzidi, unaweza kupata matatizo makubwa.

**SWALI**

Hifadhi ya Nyerere inapakana na mikoa mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Unatolewa kwenye nafasi yako lakini haikaliwi na mwingine

***KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze mada yetu kuhusu vita kwenye nafasi au cheo chako. Kwa wale wanaofuatilia mada hizi, kwenye utangulizi nilisema kwamba nafasi yoyote unayoitaka kwenye ulimwengu huu wa kawaida lazima ianze kwenye ulimwengu wa roho.***

Usihangaike kutafuta nafasi yoyote iwe ni ya kuolewa au kuoa kwenye ulimwengu huu wa damu na nyama kwani hutaipata. Nafasi yoyote nzuri unayoitaka lazima ianzie kwenye ulimwengu wa roho.

Shetani aliposhindwa kwenye ile vita maandiko yanasema "mahali pake hapakuonekana tena mbinguni. Shetani aliposhindwa, nafasi yake ilifutwa. Unaposhindwa vita vya kiroho, nafasi yako inafutwa. Nafasi yako inaweza kukuingiza kwenye vita.

Ukiona unashambuliwa sana elewa kuwa nafasi yako ni nzuri, watu wanaitamani. Yupo mfalme mmoja aliyejulikana kwa jina la Nebukadneza. Mungu alimuondoa mfalme huyu kwenye nafasi yake kwa miaka saba kutokana na kiburi lakini nafasi yake ilibaki wazi, haikupewa mtu mwingine.

Alitolewa kwenye nafasi yake ili aongezewe zaidi ya hapo alipokuwa. Mungu aliitunza nafasi yake lakini alimpitisha kwenye magumu ikiwa ni pamoja na kuishi na wanyama porini, aliyeshewa mvua na baada ya hapo akampandisha kwenye nafasi yake.

Mfalme huyu aliadhibiwa kutokana na kiburi, alitamba kwamba mji wote wa Babeli aliutengeneza kwa nguvu zake, huku akisahau kwamba yote ilikuwa ni kazi ya Mungu. Hakika, kijapo kiburi ndipo ijapo na aibu.

Wapo watu maofisini viburi vilipozidi waliondolewa kwenye nafasi zao. Wengine hujiinua kutaka wajulikane zaidi ya wakurugenzi wao. Mungu anaweza kumpa mtu cheo au utajiri akawa mfanyabiashara mkubwa lakini akishajiona amefanikiwa anasahau. Mungu anasema wazi kupitia maandiko kwamba "unapofanikiwa usinisahau".

Mpenzi msomaji, hata hivyo wapo watu kiburi kikishaondolewa Mungu ataanza kuwainua sana. Ni lazima tutambue upo wakati wa kupitia magumu na unapokataa kujishusha, kunyenyekea, kuteswa ni ishara kuwa hutafika popote.

Mungu anaweza kukuinulia mtu fulani akutese ili akuandae vizuri kwenye nafasi yako. Wengi walioinuliwa na Mungu wamepitia magumu tangu utotoni na hawakumlaumu yeyote.

Nebukadneza alirudishiwa ufahamu wake. Kila nafasi ina ufahamu na akili yake. Yupo mtu unaweza kusema naye kitu ukamgundua kuwa huyu ana akili ya chekechea. Wapo watu wana shida lakini hawawezi kuitatua, eti hajui chanzo chake. Kama hujui nani atakayekusaidia?

Unataka mafanikio lakini huna akili ya mafanikio. Kitu cha kwanza ni ufahamu. Akili yako ikisharudi na uanza kuwaza sawasawa kama vile Mungu anavyowaza, ndipo utaona upenyo. Muombe Mungu akupe akili siyo fedha kwanza. Kama huna akili hata akikupa fedha hutaweza kuzitumia. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Mpenzi msomaji, huwezi kupata nafasi yoyote kama hujapigana vita. Na ukishafanyiwa nafasi na Mungu, hakuna atakayekutoa. Na mtu aliyepania kufanikiwa hawezi kukata tamaa. Aliyekiona anachokitafuta hawezi kukiacha hadi akipate. Utakiacha kwa sababu hujakiona au hajui alichokikusudia.

Nafasi yako itaamua heshima yako, itaamua kibali chako. Kila nafasi ina heshima yake ndio maana kuna watu wanatembea na ving'ora barabarani. Usitafute kwanza heshima, anza kutafuta nafasi. Kuna nafasi huwezi kuipata kirahisi mpaka upigane, upambane.

Pia ni muhimu ukatambua kwamba Mungu anapokuinua kiroho na watu wakakujia kwa msaada usilalamike. Anafanya hivyo ili usaidie wengine.

Mungu hakupi nafasi kwa ajili yako bali kwa ajili ya wengine. Hakupi cha kwako, bali cha kwake ili umshikie kifanye kazi yake. Unapopewa nafasi itumie kujenga ufalme wake, iwe ndogo au kubwa. Mungu akiona umeanza kutumia nafasi yako kujenga ufalme wake, anakuongezea.

Kuna nafasi huwezi kuipata kwa sababu imeshikiliwa kishirikina. Lazima upigane vita kwa kubeba silaha za kiroho kupitia maombi ili ushinde. Sura ya kuolewa binti anayo, lakini yupo mtu amemshikilia mume wake katika ulimwengu wa roho. Kadhalika kijana mkewe aweza kushikiliwa kichawi.

Yamkini yupo mtu aliyetamka hautakaa uolewe au uoe. Maneno ya kinywa yana nguvu, lazima upigane vita ya kiroho kuyafuta ili uweze kujinasua katika mkwamo huo. Hakuna lisiloweze-kana kwa Mungu, yote kwake yanawezekana. Niishie hapa wiki ijayo tutasikia shuhuda. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe mfupi 0715268581.

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Mradi Bonde la Msimbazi ufuate utaalam kuondoa ubabaishaji

NOVEMBA 10, mwaka huu, Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi zilitangaza kuwa ziko katika hatua ya maandalizi ya mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia.

Mradi huo utatekelezwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), kwa kushirikiana na halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Manispaa za Kinondoni, Ubungo na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na Wakala wa Barabara (TANROADS).

Kwa mujibu wa tangazo hilo, mradi huo unatarajiwa kusaidia kukabiliana na mafuriko kwa kuwa itajengwa miundombinu itakayokuwa na uwezo mkubwa wa kupeleka maji baharini bila kutuama au kufurika katika maeneo ya bondeni.

Aidha, miundombinu hiyo itajumuisha kuimarisha kingo za mto katika maeneo korofi ili kudhibiti mmomonyoko wa udongo kwa maeneo ya kati na mwanzo wa Mto Msimbazi, kujenga makinga mchanga katika maeneo ya kimkakati, kujenga vituo na karakana za kutunza mto.

Kupitia mpango huo, kutakuwa na kazi ya kuhamisha waathirika wa mafuriko katika maeneo ya mabondeni, kuchimba na kupanua mto kuanzia barabara ya Kawawa hadi Daraja la Salender.

Pia yatajengwa matuta yenye vimo tofauti kwa ajili ya kuruhusu maji kupita kwa usalama katika kipindi cha mafuriko, kuruhusu matumizi mbalimbali ya ardhi ikiwamo City Park na uendeshaji wa maeneo ya makazi na biashara.

Lengo la tangazo hilo ni kuujulisha umma na wadau wa bonde kuwa timu za wataalam kutoka taasisi husika pamoja na wataalam washauri zinazofanua upembuzi yakinifu na usanifu zitapita katika baadhi ya maeneo ili kufanya mashauriano na wadau kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano, mahojiano na dodoso.

Hatua hiyo ni ya kupongezwa sana kwa kuwa sasa suluhisho la kudumu la bonde hilo litapatikana na sasa zile kelele za kila kipindi cha mvua hazitasikika tena.

Pia maisha ya watu wa bonde hilo yataimarika kwa kuwa hawatakuwa na hofu hata ikinyesha mvua kubwa kiasi gani au ikinyesha kwingine na kuleta udogo na uchafu mwingine ambao lengo ni kuelekea baharini.

Nawaza kwa sauti kuwa mradi huu ni mzuri lakini ni lazima utekelezwe kwa kiwango kikubwa sana ili nchi ione umuhimu wa wataalam.

Mradi huu unatukumbusha barabara ya mwendokasi ambayo katika eneo hilo ambako ni bondeni hapakuinuliwa ili barabara ipige juu ya daraja, badala yake ilipita kawaida kama eneo ambalo halina tatizo lolote.

Pia imejengwa karakana na kituo kikubwa cha mabasi ya mwendokasi ambacho kukiwa na dalili ya mvua tu wafanyakazi na watumiaji wengine wanaanza kukimbia kwa kuwa hata kama mvua imenyesha Kisarawe, basi tope na uchafu mwingine unasafirishwa kupitia Mto Msimbazi kuelekea baharini.

Kilichosikika kwenye mradi huo ni kuwa wataalam hawakusikilizwa na walilazimika kubadilisha mchoro wa awali, hali iliyowafanya hata wananchi wa kawaida kabisa ambao hawajasomea ujenzi na uhandisi kujiuliza kwamba wataalam hao hawakuona hapo ni bondeni na wahakikishe barabara inapita juu?

Kila mvua kubwa inaponyesha Dar au Kisarawe, uwe na uhakika mawasiliano kati ya upande mmoja na mwingine yanakatika kwa kuwa barabara haipitiki huku magari na miundombinu ikiharibika sana.

Sasa unakuja mradi mpya wenye lengo la kuboresha ambao unatumia fedha za Watanzania, ninaposema fedha za Watanzania ni kwa kuwa huu ni mkopo nchini inaingia ambao wanaoishi na ambao hawajazaliwa watawajibika kuulipa, ndiyo maana lazima tufuatilie matumizi na bidhaa itakayopatikana.

Haitarajiwi makosa yaliyofanyika kwenye mwendokasi yafanyike kwenye mradi huu, bali tuone thamani ya fedha na nchi kuwa na wataalam waliosoma katika ngazi mbalimbali kuanzia shahada ya kwanza hadi shahada ya uzamivu.

Ni muhimu wakajifunza kutoka nchi zilizoendelea namna zimejenga miundombinu yake kwenye maeneo kama hayo kiasi cha kuwa kivutio kikubwa cha watalii.

Kwenye nchi zilizoendelea, kuna vivutio vingi ambavyo huwafanya watu kusafiri kwenda kwenye halmashauri, manispaa na majiji kujipati fedha lakini kwetu mito imekuwa maumivu kwa kuwa mtu akiona wingu limefunga angani naye anajiandaa kufungasha kupisha maji.

Lazima mipango miji ifanye kazi kwa ustadi mkubwa pasipo kuingiliwa na wanasiasa kwa kuwa bado inakumbukwa jinsi bomoabomoa ilivyokuwa ngumu kwa kuwa wako waliokuwa wanatetea, lakini swali linakuwa inakuwaje wanaachwa wanajenga kiasi hicho?

***Tuone thamani ya fedha na miundombinu bora.***

HARUSI




Ilikuwa ni siku ya furaha kwenye maadhimisho ya Watoto Mapacha yaliyofanyika Novemba 11 mwaka huu, katika viwanja vya TCCL, Kijitonyama Dar es Salaam. Sherehe hizo zilindaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Eden Twins Foundation.















MITINDO

## TUPIA BERETI

# Mtindo wa kofia unaoshangaza

JE, umewaza wiki hii unatoka na mtindo gani wa mavazi na ukatoka bomba? Basi kama wewe ni mpenzi ya miondoko ya kisasa, unaweza kutoka tofauti kwa kuvaa kofia ya Bereti.

Kofia za Bereti zina asili ya Ufaransa, lakini kutokana na kupendwa na watu wengi zimesambaa kwa kasi katika mataifa mbalimbali, kiasi ambacho kwa sasa inatumika kama vazi muhimu hasa katika kipindi cha baridi.

Pamoja na kuwa mtindo mzuri wa mavazi, pia inatumika kama kifaa maalum cha kuhifadhi nywele zenye mafuta na kuziweka katika asili yake.

Beret ya wanawake bila shaka ni moja ya vifaa muhimu vya msimu wa baridi au nyakati za jioni wakati hali ya hewa imetulia.

Kofia ya aina hii inakuwa na rangi na mitindo tofauti, huku ikinakshiwa kwa kutengenezwa kwa ngozi ya wanyama na sufi.


Kabla ya kufikiria kununua Bereti, anza kulinganisha rangi yake kama inaendana na nywele na mavazi yako.

Wanashauri katika msimu wa joto, vaa Bereti nyepesi ambayo inaingiza hewa na kipindi cha baridi iwe nzito ili kuhifadhi joto.

Beret ya wanawake inaweza kuvaliwa kwa njia nyingi. Unaweza kuvaa ikiwa imegeuzwa kwa kufunika masikio pamoja na kuinamisha kidogo sehemu moja ya kichwa.









URЕМBO



WACHA MIDOMO ISEME

# Hizi njia za kuongeza mvuto

WATU wengi hasa wanawake, wanapenda kuwa na midomo laini yenye mvuto wa kimahaba.

Lakini kutokana na asili ya mtu na hali ya hewa, hupelekea baadhi yao kuwa na midomo iliyokauka na kuonekna haivutii.

Hata hivyo kama wewe ni mwathirika wa tatizo hili na umekata tamaa, leo tunaelekeza njia za asili na kisasa za kuitengeneza midomo yako katika mwonekana wa kuvutia.

**HATUA ZA KUFUATA**

Kunywa maji mengi, kwa sababu ukosefu wa maji mwilini ni tatizo kwa afya ya ngozi yako. Njia nzuri ya kukuza afya ya ngozi yako ni kwa kunywa maji mengi kila siku ili kukuza seli na kuweka ngozi yako hali ya unyevu.

Sugua midomo kwa kutumia vipande vya tango ambalo hutasaidia kulainisha na kung'arisha.

Tumia mafuta ya nazi kwa sababu yana matokeo mazuri katika ngozi ya binadamu.

Paka kiasi kidogo tu cha mafuta ya nazi kwenye midomo yako itasaidia kulainisha na kuiweka midomo yako katika hali ya kuvutia.

Kadhalika, paka mafuta ya petroleum jelly kabla ya kwenda kulala, itasaidia kuongeza unyevu katika midomo yake.

Tumia lipstick yenye unyevu kwa sababu zimetengenezwa kwa siagi ya kakao, siagi ya shea na mafuta ya nazi ambayo husaidia kulainisha midomo yako.

Kadhalika tumia Lip Balms zinazosaidia kukulinda kutokana na athali za mionzi ya jua.

Tumia mchanganyo wa asali na sukari, kisha paka kwenye midomo kwa dakika kadhaa.

Hii itasaidia kuiweka ngozi ya midomo yako nyororo na laini, pia husaidia kuondoa seli za ngozi zilizokufa.

Tumia vyakula vya kujenga mwili kama samaki, mayai, nyama, mboga za majani na matunda ni muhimu sana kwa afya ya ngozi yako kwani vina vitamini B na C.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Onja utamu wa karanga za mayai

KARANGA za mayai ni nzuri kwani zinatupatia virutubisho vingi muhimu kwenye mwili.

Unaweza kula kama kitafunwa na kimiminika chochote au ukala zenyewe na ukazifurahia.

Karanga za mayai ukinywa na soda, chai au juice zinaweza kukushibisha na kuufanya mlo wako wa siku.

Kwa wale wanaotaka kupunguza uzito, ukila mlo huu unaweza kupata matokeo mazuri zaidi.

**MAHITAJI**

Karanga kilo moja, yai moja, mafuta ya kupikia ya maji milimita 750, sukari vijiko sita vya chakula, unga wa ngano kikombe kimoja cha kahawa na chumvi ya unga nusu kijiko cha chai.

Mahitaji mengine ni jiko la kupikia, chombo kama bakuli au sufuria ya kuhifadhia karanga zako, mwiko au kijiko kikubwa.

**NAMNA YA KUTENGENEZA**

Chukua yai, pasua na koroga kwenye chombo kisafi.

Mimina karanga kwenye chombo ulicho koroga yai, changanya kwa kutumia mikono.

Weka chumvi kidogo, changanya vizuri, weka sukari changanya, mimina unga wa ngano, changanya vizuri.



Weka mafuta jikoni hadi yapate moto na baada ya hapo chota karanga kwa kutumia kijiko kikubwa na weka kwenye mafuta .

Endelea kuzigeuza bila kuacha hadi utakapoona karanga zimebadilika rangi kuwa kahawia.

Tumia kijiko kikubwa kuziepua na weka kwenye chombo kisafi cha wazi ili zipoe.

Funga kwenye vifuko vidogo na zihifadhi mahali pasafi tayari kwa kula na familia yao.

Unaweza pi ukatumia upishi huu kwa ajili ya kuuza na wateja wakafurahia huduma yako.


MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Ufanye nini uchumi unapotetereka katikati ya ndoto ya kujenga nyumba?

## Namna ya kuchagua muundo wa ngazi za ndani



WATU wengi wanapenda kuishi katika nyumba nadhifu na iliyobuniwa vyema. Kwa wale wenye uwezo nyumba zao wanapenda kuwa za kisasa zaidi kwa kuweka na ngazi za kuingilia vyumbani kutoka sebule kuu. Kutokana na mahitaji kuwa makubwa zifuatazo ni dondoo muhimu ya kuangalia wakati unachagua aina ya ngazi unayotaka.

**1:** Lazima mbunifu ahakikishe ngazi haziathiri ukubwa wa eneo la sebule na chumba cha kulala.

**2:** Hakikisha usalama unakuwa wa hali ya juu kwa kila rika katika familia watakaotumia ngazi. Inaweza kuwa hatari kama itatengenezwa vibaya bila kufuata vipimo sahihi.

**3:** Ngazi inatakiwa kuunganishwa katika ukuta imara ambao hautaachika haraka kutokana na matumizi ya mara kwa mara.

**4:** Hakikisha ngazi inakuwa pana ili kutoa nafasi kupita kwa urahisi endapo kutatokea dharula ambayo italazimika kutumia mtu zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja.

HALI ya uchumi inapobadilika, husababisha ukuaji au kudorora kwa maendeleo ya jamii kutokana na kuathiri uwekezaji, mwenendo wa biashara, uzalishaji na mwelekeo mzima wa kiuchumi.

Katika makala hii, tutagusia sekta ya ujenzi ambayo uchumi unapotetereka nayo huathirika na wako baadhi ya watu huahirisha kufikia malengo ya kujenga nyumba hata kama walidhamiria kwa dhati kufanya hivyo ndani ya kipindi fulani.

Peter Mshamo, ni mtaalam wa masuala ya ujenzi anayepatikana eneo la Bunju A, Dar es Salaam ambaye leo anazungumzia baadhi ya mbinu za kuzingatia kuelekea kwenye uwekezaji wa majengo kulingana na hali ya uchumi ya wakati husika.

Anasema unapokuwa na mipango ya kuanza kujenga nyumba lakini ikatokea uchumi wako kuyumba, hupaswi kuishi kwa wasiwasi au kuogopa badala yake unatakiwa kutenga muda wa kujitathimini upya kutokana na hali yako ya kifedha ya wakati husika ili kukusaidia kutimiza malengo yako hayo ya ujenzi.

Mshamo anashauri kwamba unapokumbwa na tatizo la kuyumba kwa uchumi katikati ya mipango ya ujenzi, hakikisha unakuwa makini kuepuka kutumia pesa ambayo ulikuwa umeiwekeza kwa ajili ya kazi hiyo.

"Hakikisha pesa uliyokuwa umewekeza haiguswi kwa namna yoyote. Tafuta ufumbuzi wa haraka wa kukupatia pesa nyingine ya kukusaidia kuvuka katika kipindi hicho cha uchumi kuyumba kwa ajili ya matumizi ya familia na si kugusa ile ya mipango ya ujenzi.

"Ikiwezekana, ungana na wachache ambao wameamua kwa dhati kutimiza malengo yao katika hali yoyote ile wanayokutana nayo ili upate mawazo mapya ya kukuwezesha kusonga mbele. Endelea na ujenzi taratibu bila kutumia timu kubwa ya wataalam ambao huwezi kumudu kuwalipa," anasema.






Jambo lingine anashauri kwamba katika kipindi hicho unatakiwa kubadili haraka mfumo wako wa maisha ili kumudu hali ngumu ya uchumi unayokumbana nayo kwa wakati huo na pia ikusaidie kutoharibu mipango yako ya ujenzi.

"Katika kipindi hicho ambacho unapambana kukamilisha ujenzi halafu uchumi ukayumba, unahitaji kuwa na ujasiri wa hali ya juu na kuepuka kuwa na hofu mbele ya jamii.

"Kama ulikuwa unafanya kazi kwa kulegalega, kipindi hicho unapaswa kuongeza bidii zaidi ikiwamo kuboresha kazi zako ili kukuwezesha kupata kipato cha kufanikisha malengo yako ya maisha na ujenzi. Weka zaidi juhudi kwenye kuweka akiba," anasisitiza.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
KIMFAACHO MTU CHAKE
KIKO WAPI?
MAMAAAA!
CHI NGA
NDANI YA KIBASI
WE' KONDA USHAZOEA KUNUNUA VIPIGO!
ETI KAKUBALI ANAITAMBUA TIKETI LAKINI SIO CHENJI!!
ALIPODAIWA CHENJI AKAIANDIKA NYUMA YA TIKETI ALAFU ANAKATAA KULIPA!
KAVURUGWA HUYU DOGO!
SINA MWANDIKO KAMA DAKTARI
KUCHORONGA MIANDIKO NDIO ZAO!
HII KAZI MUDA WOTE HUCHEZI MBALI NA JELA!
UKIKITUPIA KISOGO "KIAPO" MBONA JELA SIO MBALI!!!
MIE SIJAKUKATAA BALI NILIKUWA NAPIMA MAJI TU.
NDO TAYARI USHAZAMA!
MAOMBI YAKO YA KUONGEZEWA MSHAHARA YAMEFELI.
HIRIZI ZA SIKU HIZI NI FEKI!
TUNANG'ARISHA VIATU, LAKINI ROHO CHAFU
UKILETA SIKATAI KAZI
SHOE SHINE
SIKU UNGEFANIKIWA KUIVUA ROHO YAKO ILI ISAFISHWE KAMA KIATU INGEHITAJI BRASHI YA WAYA KUTAKATA!
...KINYUNYIZO CHA LEO...
...ULIVYO LEO, SIVYO UTAKAVYOKUWA KESHO...

# HABARI KIMATAIFA

## Dieng kusimamia haki Sudan

**NEW YORK,** MAREKANI

KAMISHNA mkuu wa haki za binadamu wa Umoja wa Mataifa Michelle Bachelet, jana amemteua mwanasheria wa Senegal Adama Dieng, kama mtaalamu wa haki za binadamu nchini Sudan.

Uteuzi huo unafuatia mapinduzi ya kijeshi yaliyotokea nchini humo mwezi uliopita.

Bachelet alisema kwamba Dieng ataanza kutekeleza majukumu yake mara moja, na muda wake utamalizika baada ya kurejeshwa kwa serikali inayoongozwa na raia.

Dieng mwenye umri wa miaka 71, ni mjumbe wa Baraza la Ndani la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa.

Baraza hilo linaunga mkono ukosoaji wa kimataifa wa mapinduzi ya Sudan ya tarehe 25 Oktoba, wakati Jenerali Abdel Fattah al-Burhan alipoivunja serikali na kutangaza hali ya hatari nchini kote.

Mapinduzi hayo yamepelekea kuzuka maandamano ya nchi nzima pamoja na ghasia zilizosababisha vifo vya takriban watu 14, kulingana na madaktari.

**DW.**

## Ufaransa yaionya Urusi kuhusu Mali

**PARIS,** UFARANSA

UFARANSA imeionya Urusi, kuacha kutuma mamluki wa kijeshi kutoka kampuni yake Wagner kwenda katika ukanda wa Sahelo-Sahara nchini Mali, ikisema jambo hilo halitakubalika.

Hayo yalisemwa na mawaziri wa Mambo ya Nje na Vikosi vya Wanajeshi wa Ufaransa , Jean-Yves Le Drian na Florence Parly, wakati wa mahojiano mjini Paris na wenzao wa Urusi, Sergei Lavrov na Sergei Choïgou.

Katika mkutano huo walisisitiza kuhusu hatari za uharibifu wa kikanda na mashambulizi dhidi ya maslahi ya Ufaransa na washirika wake wanaohusika katika mapambano dhidi ya ugaidi katika ukanda wa Sahel.

Tamko hilo inatokana na taarifa ya viongozi wa kijeshi wa Mali walioko madarakani wakitishia kutumia huduma za kampuni ya kibinafsi ya Wagner, ambayo inaelezwa kuwa karibu na Rais wa Urusi, Vladimir Putin. Kampuni ya Wagner tayari ipo barani Afrika, katika nchi za Libya na Jamhuri ya Afrika ya Kati, ambako kunaripotiwa kunatekelezwa vitendo vya uhalifu dhidi ya raia.

Makubaliano ambayo yanajadiliwa kulingana na shirika la habari la Reuters, yatahusu kutuma mamluki kadhaa au hata mamluki elfu moja wa Urusi kwenda Mali.

Kampuni ya Wagner inasemekana italipwa faranga za bilioni sita au zaidi ya euro milioni tisa kwa mwezi kwa kufundisha wanajeshi wa Mali na kutoa ulinzi kwa viongozi wengine wakuu.

Hivi karibuni shirika la habari la Reuters, limenukuu vyanzo saba vya kidiplomasia na vya kijeshi, lakini hakuna uthibitisho rasmi, kutoka kwa kampuni ya Wagner au upande wa mamlaka nchini Mali.

**RFI.**

# Uchaguzi Libya kufanyika Des 24

**PARIS,** UFARANSA

VIONGOZI wa mataifa mbalimbali waliohudhuria mkutano wa kuisaidia Libya kufanya uchaguzi, wametishia kuwawekea vikwazo watu watakaovuruga mchakato wa kumchagua rais wa nchi hiyo.

Katika mkutano huo uliofanyika nchini Ufaransa, umepanga uchaguzi huo kufanyika Desemba 24, mwaka huu.

Sehemu ya tamko la viongozi hao, limewatolea wito wadau kuhamasisha kufanyika kwa uchaguzi huo wa rais na wabunge katika njia ya huru, haki na ambao utajumuisha pande zote.

Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, ambaye alikuwa mwenyeji wa mkutano huo, pia wakuu wengine wa nchi walioudhuria ni Angela Merkel wa Ujerumani, makamu wa rais wa Marekani, Kamala Harris na viongozi wa Libya, Misri na Italia. Mpango unaoungwa mkono na Umoja wa Mataifa ni wa kufanyika kwa uchaguzi mwezi ujao nchini Libya, taifa lililokumbwa na machafuko tangu vuguvugu lililosababisha kuondolewa madarakani kwa kiongozi wa muda mrefu Moammar Gadhafi mwaka 2011.

Umoja wa Mataifa inauchukulia mpango huo kama msingi muhimu wa kurejesha utulivu nchini humo baada ya muda mrefu wa machafuko na mzozo.

Hata hivyo, Urusi na Uturuki walipeleka wawakilishi wa ngazi ya chini licha ya mialiko ya wakuu wa mataifa hayo kwenye mkutano huo.

Uturuki ina wasiwasi kwamba Ufaransa huenda ikataka kuondoka kwa majeshi yake nchini Libya.

Urusi inawaunga mkono vikosi vya Libyan National Army vilivyojikita mashariki mwa nchi hiyo na vinavyosaidiwa na Umoja wa Falme za Kiarabu na Misri.

**DW**



Wafanyakazi wa kusafirisha vifurushi wakionekana kuzidiwa na shehena ya vitu vilivyonunuliwa na watu mbalimbali mjini Beijing wakati wa sherehe ya siku ya mabachela inayofanyika kila mwaka nchini China. **PICHA: REUTERS**

# Msiri wa Trump, ashtakiwa kuficha ukweli

**WASHINGTON,** MAREKANI

ALIYEKUWA mkuu wa mikakati wa Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump, ameshtakiwa kwa kukataa kutoa ushahidi mbele ya kamati ya uchunguzi kuhusu uvamizi wa majengo ya Bunge uliotokea mwezi Januari.

Steve Bannon, anashutumiwa kwa kutowasilisha nyaraka za ushahidi zilizoombwa na kamati hiyo, kulingana na Idara ya Sheria ya mjini Washington. Kamati hiyo iliyoundwa na Baraza la Wawakilishi inapaswa kuchunguza sababu ya shambulio hilo lililofanywa na wafuasi wa Trump na Bannon anatazamwa kama shahidi mkuu. Inasemekana alijua mapema kwamba kutatokea vurugu mnamo Januari 6, mwaka huu.

Trump aliishtaki kamati hiyo pamoja na kuitaka Idara ya Kumbukumbu za Taifa kuzuia kutolewa kwa nyaraka mbalimbali za ushahidi, lakini Jaji Tanya Chutkan ameunga mkono kauli ya Rais Joe Biden, na kuamuru wiki hii kwamba marais sio wafalme na wanapaswa kushtakiwa.

**DW.**

# Marekani yaiwekea vikwazo Eritrea

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imewawekea vikwazo wanajeshi wa Eritrea, kwa kujihusisha na mzozo unaoendelea kwenye taifa jirani la Ethiopia.

Katika mzozo huo kumesababisha maelfu ya watu kuuawa na wengine kukimbia makazi yao.

Wizara ya fedha ya Marekani, ilisema imechukua hatua hiyo kufuatia ripoti kadhaa za vitendo vya uporaji wa vyakula, unyanyasaji wa kingono, mauaji ya raia na kuzuia misaada ya kiutu vinavyofanywa na wanajeshi wa Eritrea.

Vikwazo hivyo vimemgusa pia mkuu wa ofisi ya usalama wa taifa hilo, Abraha Kassa Nemariam, kampuni zinazosimamia biashara na maslahi ya kifedha ya chama tawala na mtendaji mkuu wa ushirika Hagos Ghebrehiwet W. Kidan.

Aidha Marekani imeonya kiuwekea vikwazo serikali ya Eritrea na vikosi vya upinzani kwenye jimbo la Tigray nchini Ethiopia, iwapo hakutapigwa hatua yoyote ya kusitisha mapigano na kuanzisha mazungumzo.

**DW**

MAKALA

# WASIOFAHAMIANA WALIDUMU KULIKO TULIVYO LEO



Na Magabilo Masambu

NI ukweli usiopingika kwamba Uhusiano wa kindoa au kimapenzi leo hii umekuwa kizungumkuti. Inawezekana maswali ni mengi kuliko majibu huku kila mmoja akijiiuliza sababu hasa ni nini. Wako wanaosema pengine malezi ya leo si sawa na yale ya zamani. Lakini tunajiuliza hivi wale waliokuwa wakilea zamani siku hizi wameisha? Wapo nao wanashangaa.

Lakini ukweli kwamba wale waliokuwa wakioana bila kufahamiana ndiyo waliodumu kwenye ndoa zao kwa miaka mingi zaidi, huwezi kupingwa. Ninaposema hawakuwa wanafahamiana namaanisha kwamba wake au waume walikuwa wakitafutwa na wazazi husika au ndugu.

Wale wanaofahamiana leo namaanisha mme na mke wanakutana kabla ya wazazi kuwafahamu, kisha wanabebana na kupelekana kwa wazazi.

Zamani, wazazi ndio walifahamiana kwanza kabla ya wahusika. Lilikuwa jambo la kawaida sana mtoto wa kiume kutoka katika matembezi yake au shuleni anaporejea nyumbani, kukuta ameshaletewa binti wa kuoa!

Nimewahi kupata hadithi juu ya babu na bibi yangu walivyooana. Babu alikuwa anasoma wakati huo akiwa darasa la nne, siku moja karudi nyumbani anakuta binti pale hakuwa na wasiwasi maana alijua tu labda ni ndugu yetu amekuja kutusalimia. Siku ya kwanza ikapita, akaenda shuleni na kumwacha binti nyumbani na hakuambwa chochote.

Siku ya pili katoka shule ilipofika jioni, anaitwa na wazee akaambiwa: "Unamwona yule binti? Akasema namwona. Akaulizwa unamwonaje? Hakuwa ameelewa akasema namwona tu. Basi akaambiwa tangu leo huyo ndiye mkeo." Majadala ukafungwa hakuna cha kujitetea, ndoa yao ikazaliwa tangu siku hiyo. Wazee hawa wameishi pamoja zaidi ya miaka 60 mpaka pale babu yangu alipotwaliwa na kumwacha bibi yangu.

Leo tunaonana wenyewe na kwamba tumechaguana na tunapendana kwelikweli. Nilichogundua ni kwamba upendo wa leo unafanana na moto wa mabuwa ya mahindi ambao hulipuka kwa nguvu na kwisha mara moja. Lakini mapenzi ya zamani najaribu kuyafananisha na moto wa kisiki, ambao unawaka taratibu huku ukichukua muda mrefu kuzima.

Kuna wakati nimejaribu kufikiri kwamba pengine mwingiliano wa mila na desturi labda nao umeleta shida, lakini katika kufanya kauchunguzi kangu nikagundua kwamba hata watu wa jamii moja leo kudumu ni hadithi nzito. Watabebana huko wanazungumza lugha moja, lakini utasikia baada ya siku chache hawako pamoja.

Wako wanaosema hata hizo ndoa tunazosema waliishi sana, waliishi kwa kuvumilia mambo mengi ndani ya ndoa zao na kwamba kilichokuwa kinawafanya waishi zaidi ni kuheshimu yale makubaliano ya wazee walio waunganisha. Walifika mbali zaidi kuonekana kwamba kuachana ilikuwa aibu kwa jamii nzima, hivyo kuwafanya watu waishi pamoja wakiwa hawapendani bali kulinda mira na desturi.

Najaribu kufikiri, pengine wavumilivu wamekosekana kwenye jamii zetu au kizazi chetu hiki hatuthamini mila na desturi za jamii zetu tena? Kama kuchaguliwa mume au mke, lilikuwa jambo baya kwa nini tunaochaguana leo lakini hatuishi pamoja?

Wengine wanasema mapenzi leo yamekuwa rahisi sana kiasi cha kufanana na mtu kuingia dukani na kununua 'big-G' kuitafuna na kuitema. Inawezekana ni kweli kwamba kinachopatikana kwa urahisi huwa kinapotea kirahisi pia. Zamani ilikuwa kazi ngumu sana kuanzisha uhusiano. Kwanza namna ya kuwasiliana ilikuwa ngumu, binti kama hujamvizia kisimani labda mmekutana machungani lakini siku hizi uhusiano asubuhi saa 2:00, saa 4:00 ndoa!

Haimaanishi kwamba wale wote wanaoonana wenyewe wanaachana bado wapo wanaodumu. Si kweli pia kwamba wale waliokuwa wanatafutiwa walidumu wote lakini tunajaribu kutazama kwa wingi wake inaonekana leo tuaachana zaidi. Madhara yake ni kuwa na watoto wengi wa mitaani na kuwabebesha babu na bibi zetu wajukuu ambao hawakustahili kuwalea, maana wao walitulea sisi.

Huu utaratibu wa kutafutiwa pengine ndiyo ilikuwa njia sahihi zaidi maana maandiko yanasema: "Si vyema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni na kila ndege wa angani akamletea Adamu ili aone atawaitaje kila kiumbe hai jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake (Mwanaume ndiye anayetakiwa kutoa jina la mtoto lakini siku hizi kuna mambo ya haki sawa haya bana)

Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa na ndege wa angani na kila mnyama wa mwituni, lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye. Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito naye akalala kisha akatwaa ubavu wake mmoja akafunika nyama mahali pake ule ubavu akaufanya mwanamke akamleta kwa Adamu"

Najaribu kutafakari kwa nini Mungu hakuwaumba watu wawili baadae waje wakutane na waoane, tunaona hata Adamu aliletewa mwanamke hakutafuta mwenyewe ndiyo maana baadhi ya watu wanasema inawezekana mipango ya ndoa tunaikosea mwanzo kabla ya kuanza.

Sababu nyingine inatajwa kuwa ni uchumi. Wako wanaotamani maisha ya haraka haraka wasipoyaona wanakimbia lakini pia na nia ya mwanzo kwa nini uwe na fulani yale mategemeo yasipoonekana mapema basi ndoa inakuwa ndoano.

Wengine wanadai ahadi nazo zimekuwa chanzo kwamba vijana wanaahidi mambo yasiotekelezeka kuiga na kujifunza kutoka kwenye ndoa zingine. Watu hawa wanasema ndoa ni jambo la kipekee halistahili kujifunzwa kutoka kwa mwingine kwasababu changamoto hazifanani mambo ni mengi muda mchache.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Tukuyu, MECCO zilivyozitikisa Simba, Yanga



Na Adam Fungamwango

KWA miaka mingi Mkoa wa Mbeya umekuwa ukitoa timu tishio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Si kama mikoa mingine haijawahi kutoa, bali mkoa huo umeendelea kutoa vikosi vya timu ambazo hata kama hazijachukua ubingwa. Zimekuwa imara na kuogofya si kwa timu zinazocheza Ligi Kuu lakini hata kwa timu kongwe zinazopishana kutwaa ubingwa, Simba na Yanga.

Mfano kwa sasa Mkoa wa Mbeya una timu tatu za Ligi Kuu ambazo ni Mbeya City, Prisons na Mbeya Kwanza ambayo imepanda msimu huu. Ni nadra sana kwa Ligi Kuu Tanzania Bara kuchezwa bila kuwa na timu kutoka Mbeya, kama ilivyo kwa Dar es Salaam. Kuna wakati ligi ilichezwa bila ya kuwa na timu kutoka Morogoro, Tanga, au Mwanza, mikoa ambayo inajitahidi sana kutoa timu za Ligi Kuu.

Mkoa wa Mbeya unafanana na Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwa na timu za Ligi Kuu. Mfano msimu huu Dar ina timu za Simba, Yanga, KMC na Azam na Mbeya wakiwa na Mbeya City, Mbeya Kwanza na Prisons, ingawa kwa sasa maafande hao wanatumia Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga kwenye mechi zake za Ligi Kuu ili tu kuepusha msongamano.

Kama Ihefu FC isingeshuka, basi mkoa huo ungekuwa na timu nne kwenye Ligi Kuu, na kuwa mkoa wa kwanza kuwa na timu nyingi kwenye msimu mmoja kuizidi Dar es Salaam. Hii ina maana kwamba hata msimu uliopita, Mbeya ilikuwa na timu tatu, kabla ya Mbeya Kwanza kupanda.

Pamoja kupanda kwa mara ya kwanza, Mbeya Kwanza inaonekana kama timu zoefu, kwani hata ukiifunga mabao mawili usidhani umemaliza mechi. Mabao hayo yanaweza kurudi yote kama walivyofanya kwa ndugu zao Mbeya City waliporudisha mabao yote mawili ya kuwa sare ya mabao 2-2. Lakini pia Polisi Tanzania ambayo iliongoza mabao 2-0 hadi mapumziko, yalirudi ndani ya dakika tano.

Tunakumbuka kuwa Mbeya City ilipopanda Ligi Kuu ilivyokuwa ni timu ya namna gani.

Tunakumbuka msimu wa 2013/14 ilipopanda Ligi Kuu, ikavihenyesha vigogo vya soka nchini, Simba, Yanga na Azam kiasi kwamba haikushangaza iliposhika nafasi ya tatu msimu huo na msimu uliofuata ikashika nafasi ya nne.

Ndiyo timu iliyokuwa na mashabiki wengi ukiondoa Simba na Yanga, mitaani wakivaa jezi zao na mashabiki wao wakisafiri popote pale timu yao inapokwenda kucheza.

Prisons sina haja ya kuielezea. Pamoja na kwamba yenyewe inacheza tu ili ibaki Ligi Kuu, imekuwa ikizipa mechi ngumu Simba na Yanga pia kuwahi kuchukua ubingwa wa Jamhuri ya Muungano mwaka 1999 na kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika, sasa maarufu kama Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kabla ya timu hizo, huko nyuma kuna timu za Tukuyu Stars na MECCO zote za Mbeya, zilifanya maajabu ambayo hadi leo yanaendelea kukumbukwa na kuandikwa kwenye historia ya soka. Ni historia ambayo inaendelea kuupaisha Mkoa wa Mbeya hadi leo.

Mwaka 1986, timu ya Tukuyu Stars ya Mbeya, ilipanda daraja na moja kwa moja ikatwaa ubingwa na Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara (kabla ya kubadilishwa na kuitwa ligi kuu ilivyo sasa).

Ikawa ni rekodi ya aina yake ya timu kupanda na kuchua ubingwa. Jambo hili liliziumiza timu za Simba na Yanga. Kama kawaida yao, walichofanya ni kuisambaratisha. Wanagawana wachezaji wa timu hiyo, wengi walichukuliwa na Yanga, wengine wakaenda Simba.

Zilifanya hivyo kwanza ili kupata wachezaji wazuri kwa sababu Tukuyu ilionekana kuwa na wachezaji wenye uwezo mkubwa. Pili ni kuinyong'onyesha timu hiyo kwani wangeiachia, ingeweza kuchukua tena mara ya pili. Kilichotokea ni kwamba Tukuyu ikashuka daraja baada ya wachezaji wake wengi mastaa kuchukuliwa.

Baadhi ya wachezaji wa Tukuyu Stars waliowika ni Mbwana Makata ambaye kwa sasa ni kocha wa Dodoma Jiji, aliyekuwa golikipa, Ally Kimwaga, Michael Kidilu, baadaye akaenda Simba, Godwin Aswile aliyechukuwa na Yanga, baadaye kujiunga na Simba, Selemani Mathew Luongo, alijiunga na Yanga, baadaye naye akaenda Simba, Aston Pardon, aliyemalizia soka Simba, Salum Kabunda aliyekwenda Yanga, Justin Mketeke naye alikwenda Yanga, Karabi Mrisho, Richard Lumumba, Peter Mwakibibi na Kelvin Haule ambaye naye alikwenda kujiunga na Simba.

Wengine ni John Alex aliyekwenda Yanga na Yusuph Kamba. Hiki kilikuwa kikosi cha dhahabu cha Tukuyu Stars.

Baada ya kufanyiwa figisu na kushuka daraja, ikaja timu nyingine ya Mbeya, inaitwa Mecco. Ilikuwa inamilikiwa na Kampuni ya Ujenzi ya MECCO. Ilikuwa balaa. Haikuchukua ubingwa, lakini ilikuwa timu tishio kiasi cha klabu za Simba na Yanga kuogopa hata kucheza nayo.

Waliituhumu kuwa wachezaji wao wanatumia dawa za kuongeza nguvu kutokana na stamina, kasi na kutochoka kwa dakika zote 90. Ilisemekana ilikuwa na uwezo wa kucheza hata dakika 200 bila kuchoka.

Ilikuwa ni mtihani mzito kucheza na timu hiyo, ambayo inasemekama ni mazoezi ya milimani, hali ya hewa na Mbeya na aina ya vyakula, ndivyo vilivyokuwa vikifanya wachezaji wa timu hiyo kuwa hivyo. Na hata walipopimwa ilionekana hawatumii madawa.

Nayo ilitamba kuanzia mwaka 1990. Baadhi ya wachezaji wake wasiosahaulika ni George Mangula aliyekuwa langoni, Rashid Mandanje, Gabriel Mwitika, Mbaga Mwantiku, Charles Makwaza, mkoba na nahodha wa timu, Danford Ngessi, Abeid Kasabalala, John Kanyiki, Betwel Afrika, Ephraim Kayeta na Nassib Abass. Wachezaji wa akiba walikuwa ni Juma Hamadi, Jaffar Nyoni, Idd Mzomwe na Augutine Sanga.

# HADITHI

# Ajenda ya siri-4

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je, ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

SIJAWAHI kumuona na pesa zingine zaidi ya zile alizokuwa akilipwa. Kama angekuwa na pesa zaidi mimi ningejua. Labda wawe wamemdanganya watampa, halafu hawajampa."

"Unaamini kweli Tina amemuua Chilambo kwa kumuwekea sumu kwenye chakula?"

"Baba, mahakama imeshasema, sasa mtu kama mimi nitasema nini tena. Ila inaniuma, halafu sielewi, hivi kweli Tina ninayemjua mimi? Labda kwa sababu moyo wa mtu ni kichaka."

"Pia kuna dhana alikuwa hajalipwa mshahara miezi sita, ni kweli?"

"Si kweli." Swali hili alijibu mzee Digalu.

"Pesa zake za kila mwezi alinipa mimi nimuwekee, zingine nilimwambia afungue akaunti benki aweke, kwa hilo hapata."

"Zingine nilikuwa nalipwa mimi, si nilikwambia na mimi nilikuwa napewa kama kifuta jasho kutokana na kuwapa msichana wangu. Tulikuwa tunalipwa kila mwezi." Mama Mwasi alidakia.

Tayari gari lilikuwa limeshafika maeneo ya Tandale kwa Mtogole. Alichofanya Eddy ni kuhakikisha anaifahamu nyumba ya mzee Digalu.


*************************

Aliamka asubuhi kichwa kikiwa kinamuuma. Akakumbuka kuwa alikuwa anaota. Lakini alikuwa amesahau nini alichokuwa anaota. Alichokuwa na uhakika nacho ni kwamba haikuwa ndoto ya kawaida.

Kabla hajatia chochote kinywani, alichukua vidonge vya kutuliza maumivu, akameza na kushushaa na glasi ya maji.

Dakika mbili baadaye ndipo picha ilipoanza kumjia ya kile ambacho alikuwa anaota. Ni kwamba mtu alikuwa analia. "Ni nani yule?" Alijiuliza mwenyewe.

Akakumbuka kuwa ilikuwa ni sura ya msichana. Ndiyo, alikuwa ni msichana aliyekuwa analia. Picha nzima kama mkanda wa video ukaanza kurudia kwenye ubongo wake. Ni kwamba alikuwa katikati ya umati wa watu. Kwa mbali alisikia sauti ya msichana aliyekuwa analia. Aliwapita watu wote waliokuwa kwenye umati huo. Akaja kuanguka kwenye miguu yake na kulia kwa sauti ya huruma "nisaidie nisaidie." Wakati anajiuliza ni kwa nini amewapita wote wale kwa kuja kwake? Ina maana watu wote wale hakuona mtu yeyote wa kumsaidia? Alijuaje kama yeye ndiye anaweza kumsaidia pekee? Kama hajafanya chochote akaamka ghafla, jasho likiwa linamtoka.




**Alidhania ni kwamba huenda ndoto ile ilitokana na tukio la kumuona msichana Tina Kauzeni alipokuwa akilia mahakamani baada ya kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa. Ikaongezewa na kuwapa lifti walezi wake hadi nyumbani kwao, huku wakimpa historia nzima ya msichana yule.**

Kila akijenga picha ya msichana yule, bado hakumbuki kama alishawahi kuona sura yake.

Pamoja na hayo haikumsumbua sana kwa sababu, Eddy huwa haamini sana ndoto.

Alidhania ni kwamba huenda ndoto ile ilitokana na tukio la kumuona msichana Tina Kauzeni alipokuwa akilia mahakamani baada ya kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa. Ikaongezewa na kuwapa lifti walezi wake hadi nyumbani kwao, huku wakimpa historia nzima ya msichana yule.

Kwa hiyo ndoto ile ilitokana na mlolongo wa matukio yale, na wala haikuwa na maana nyingine yoyote ile.

Alienda kuoga, aliporejea alivaa nguo zake kwa ajili ya kwenda ofisini. Kabla hajaondoka alimpigia simu rafiki yake Florence Tinga, wakili ambaye jana yake alikuwa ofisini kwake.

"Niambie Eddy." Tinga alidakia baada ya simu kupigwa.

"Yale ya kiofisi ya jana tumemaliza, kuna jambo moja nilitaka unisaidie Tinga."

"Lipi hilo Eddy, ushaanza mambo yako.

"Hapana, sio mambo yetu yale."

"Ahaa, maana wewe, nikajua labda jana umeona mtoto mkali, unataka nikuunganishie." "Hahahaha, hapana. Nilichotaka kukwambia kinahusiana na ile kesi ya yule binti jana."

"Binti gani? Ahaa yule aliyehukumiwa kunyongwa?"

"Ndiyo. Naomba kitu kimoja. Nadhani wewe ulikuwapo wakati kesi hii ilipoanza hadi alipohukumiwa sawa?"

"Ndiyo."

"Naomba tu japo kwa ufupi mwenendo ulivyokuwa sawa?"

"Okay, basi kitakupatia, nitakutumia kwenye barua pepe yako sawa?"

"Sawa nikutakie asubuhi njema Tinga."

"Okay nawe kazi njema, baadaye."

**********************************

Ilikuwa ni siku ya Ijumaa. Ilionekana ni kama siku nyingine zote. Haikuonekana kama inaweza kuwa siku mbaya. Siku ya balaa.

Tina Kauzeni aliamka na kufanya kazi zake kama ilivyo siku zote. Ilipofika saa tano asubuhi aliondoka nyumbani hapo. Alirejea baada ya kupita saa nzima. Ilipofika saa nane aliondoka tena nyumbani hapo kwa tajiri yake Hafidh Chilambo. Safari hii alitumia saa mbili. Alirejea nyumbani saa 10:00 jioni.

Majira ya saa 10:15, robo saa baada ya kurejea, Chilambo alirejea nyumbani.

Inasemekana kuwa sio kawaida sana ya Tina kuondoka nyumbani. Huondoka kwa nadra sana na hata kutumwa na mabosi wake, yaani baba na mama ilikuwa ni mara chache sana. Mara nyingi wanaotumwa safari za nje kwenda madukani, sokoni wakati mwingine ni hausiboi au mlinzi wa getini. Siku hiyo kulikuwa na mlinzi pekee, hausiboi alikuwa amepata udhuru, alisafiri kwenda kwao.

Hata hivyo, mahakama iliambiwa kuwa hakutumwa na mtu yeyote yule, alikuwa akiondoka tu mwenyewe jambo ambalo si la kawaida.

Siku ya tukio, mke wa Chilambo, bi Hellen, tangu saa nne asubuhi alikuwa ameondoka nyumbani hapo na watoto wake wawili, Prisca na Paul, akiwapeleka kwa shangazi yao Temeke.

Siku hiyo hiyo jioni yake, Hellen Chilambo alikuwa amealikwa kwenye sherehe za harusi zilizofanyika kwenye hoteli moja Sinza, Dar es Salaam.

Kwa maana hiyo kuanzia saa nne asubuhi, hakuwapo nyumbani hadi alipopata taarifa za kufariki kwa mumewe akiwa kwenye harusi.

Mahakama ikaambiwa kuwa kutokana na kutokuwapo kwa mke wa marehemu, mshtakiwa alipata fursa ya kutekeleza azma yake hiyo kirahisi zaidi.

Chilambo alianza kula chakula hicho saa 11:00 jioni kwa sababu alichelewa kurejea nyumbani, na hata alipofika bado kuna vitu vingine alikuwa akivifanya. Baada ya nusu saa alianza kujisikia vibaya, lakini alidhani tumbo tu la kawaida. Kiliandaliwa, kikapikwa na kuwekwa mezani na mshtakiwa Tina Kauzeni.


Hali ilianza kuwa mbaya kadri muda ulivyokuwa unazidi kwenda na alifariki saa 2:00 usiku akiwa amefikishwa kwenye Hospitali ya Mwananyamala.

Ushahidi uliendelea mahakamani ulieleza kuwa uchunguzi wa awali ulionyesha kuwa Chilambo alifariki baada ya kula chakula ambacho kilikuwa na viashiria vya sumu. Kabla ya mazishi, daktari Thomas Mtuta, aliuchunguza mwili wa marehemu na kugundua kuwa ndani ya chakula alichokula, kuliwekwa aina mbili za dawa baridi ambazo si chungu, lakini zikichanganywa na mtu akinywa kwa kuwekewa kwenye kinywaji, au chakula, basi anaweza kupoteza maisha saa mbili au tatu baada ya kunywa, na athari zinaanza kuonekana kiasi cha nusu saa tu baada ya kuingia mwilini.

Mshtakiwa mwenyewe alikiri vyote, lakini alijitetea kuwa hakujua kama chakula hicho kina sumu au dawa yoyote iliyowekwa.

Alipoulizwa kwa nini sio yeye wakati siku hiyo alikuwa yuko peke yake kuanzia saa nne asubuhi, alishindwa kujibu.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# HARMORAPA AMSHANGAA RHINO KUJIZUSHIA KIFO

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Hamorapa, amesema taarifa za kifo cha msanii Rhino King, zilizosambaa kuwa za uongo ni kama kutafuta kiki kwa mashabiki.

Harmorapa, amesema kujitangazia kifo wakati mtu yupo hai ni sawa na kumtania Mungu, japo alifanya hivyo kama kuwandaa mashabiki wake kwa ajili ya kazi yake mpya.


Hii sio mara ya kwanza kwa msanii kutafuta kiki kwa kujitangazia akifo, msanii wa singeli Meja Kunta naye aliwahi kujizushia kifo mwaka 2020.

# Mbosso, Zuchu hawashikiki

WIMBO unaolalamikiwa na mwanamuziki kutoka Kenya, ulioimbwa na wasanii kutoka WBC, Mbosso na Zuchu 'For Your Love' unazidi kutesa katika mitandao ya muziki duniani.

Hivi karibuni, Otile Brown wa Kenya, amedai kuibiwa melodi za wimbo wake 'baby love' na kutumika katika wimbo wa Mbosso bila ridhaa yake.

Mpaka jana wimbo huo umekuwa ukikimbiza katika mtandao wa You Tube, kwa kuangaliwa wa watu wanaokaribia milioni moja, huku ukishika nafasi za juu.



# Jitu Baya ajitambulisha 'Mikoa Yote'

RAPA anayekuja kwa kasi, Jitu Baya, ametambulisha singo yake nyingine inayoitwa 'Mikoa Yote' maalum kwa mashabiki wake wa mikoani.

Akizungumza na Nipashe, Jitu Baya, amesema wimbo huo ambao amemshirikisha msanii chipukizi Katembo, ameuandaa kwa ajili ya kuwashukuru mashabiki wake kutoka sehemu tofauti ya Tanzania kwa kuumunga mkono.

"Nilianza nikiwa na mashabiki wachache hapa mtaani kwetu, lakini sasa nina watu wengi wananiunga mkono na ili kutoa shukrani zangu nimetunga wimbo huu 'Mikoa Yote" kuonyesha nawathamini," amesema Jitu Baya.

Msanii huyo ambaye anafananishwa na rapa maarufu, Chidi Benz, amekuwa gumzo kutokana na umahiri wake katika muziki wa Hip hop.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WERNER ATAKIWA BARCA

BARCELONA wanamsaka mshambuliaji wa Chelsea, Timo Werner, 25, na watajaribu kumnasa kwa mkopo nyota huyo wa zamani wa RB Leipzig Januari. Werner ameanza mechi nne tu za ligi kuu England msimu huu. ***(Marca)***

### STERLING HAUZWI

MANCHESTER City itakataa jaribio lolote kutoka Barcelona la kumsajili, Raheem Sterling, 26, Januari. Barca wamekua wakihusishwa na mshambuliaji huyo wa England ambaye ameamza michezo mitatu tu ya ligi Kuu England msimu huu. ***(ESPN)***

### CITY WAKOMAA NA KANE

MANCHESTER City wanajiandaa kuijaribu tena Tottenham Hotspur Januari kwa kupeleka ndoano kwa ajili ya mshambuliaji wa England, Harry Kane, 28, baada ya kushindwa kumsajili nyota huyo katika majira ya joto. ***(ESPN)***

### ZIYECH KUTUA DORTMUND

WINGA wa Chelsea, Hakim Ziyech, 28, raia wa Morocco, anaweza kujiunga na Borussia Dortmund Januari, ikiwa ni miezi 18 tangu ajiunge na Blues akitokea Ajax kwa ada ya pauni milioni 33. ***(Mirror)***

### KOUNDE KUBAKISHWA

KLABU ya Sevilla inapambana kumbakisha mlinzi wake, Jules Kounde, 23, hadi majira yajayo ya kiangazi licha ya kusakwa na Manchester United. ***(Marca)***

### KETELAERE AWANIWA SPURS

TOTTENHAM Hotspur inamtaka mshambuliaji wa Club Bruges, Charles de Ketelaere, 20, raia wa Ubelgiji, lakini inakabiliwa na ushindani kutoka kwa AC Milan kwa ajili ya kinda huyo. ***(Calciomercato)***

### TRAORE ASAKWA VALENCIA

WINGA wa Klabu ya Wolves, Adama Traore, 25, raia wa Hispania, anasakwa na Valencia.***(Sun)***

### DALOT KUBAKI MAN UNITED

MLINZI wa Ureno, Diogo Dalot, 22, ana matumaini ya kubaki Manchester United licha ya kusakwa na AS Roma, ambao wanafundishwa na Jose Mourinho. Kocha huyo raia wa Ureno alimsajili nyota huyo na kumpeleka Old Trafford mwaka 2018. ***(Caught Offside)***


### SMITH KUIBUKIA NORWICH

DEAN Smith, aliyetimuliwa na Aston Villa jumapili iliyopita, anatarajiwa kurejea haraka kufundisha baada ya Norwich City kushindwana na Frank Lampard. ***(Sun)***

### HENDERSON KUONDOKA

GOLIKIPA wa England, Dean Henderson, 24, anatarajiwa kuondoka Manchester United baada ya kushindwa kuwa kipa namba moja dhidi ya David de Gea. Henderson ameanza mchezo mmoja tu msimu huu. ***(Mail)***

## DONDOO MAGAZETI




# BARCA YAMSAJILI TENA DANI ALVES

## Ametua kwa uhamisho huru, lakini hatacheza hadi Januari...

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imefikia makubaliano ya kumsajili tena Dani Alves kwa uhamisho huru baada ya kuondoka katika Klabu yake ya sasa, Sao Paulo ya nchini Brazil.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anarudi Camp Nou miaka mitano na nusu baada ya kuondoka ambapo alicheza kwa misimu nane na miamba hao wa Katalunya, ingawa hataruhusiwa kucheza hadi Januari mwakani.**

Alves alishinda mataji 23 katika kipindi chake cha kwanza kukaa hapo Barcelona kabla ya kwenda Juventus kwa msimu mmoja, akacheza misimu miwili kule Paris Saint-Germain na miaka miwili iliyopita alikuwa kule Sao Paulo.

Alikuwa jukwaani wakati Barca ikishinda bao 1-0 dhidi ya Dynamo Kiev Novemba 2 kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya na klabu hiyo ya La-Liga ilithibitisha Ijumaa kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38 anarudi kwenye kikosi hicho kama mchezaji huru.

Miezi miwili baada ya kuondoka Sao Paulo kutokana na matatizo ya kimkataba, Alves amesaini na Barca mkataba ambao utamuweka hapo hadi mwishoni mwa msimu huu.

Kurudi kwa Alves kumekuja wiki moja baada ya gwiji wa Klabu hiyo, Xavi, kuteuliwa kuwa kocha mpya wa Barcelona na imeripotiwa kuwa mchezaji mwenzake huyo wa zamani ndio aliyechangia kwa kiasi kikubwa kukamilishwa kwa uhamisho huo.

Mlinzi huyo mkongwe alicheza mechi 247 akiwa na Barca baada ya kujiunga nayo akitokea Sevilla mwaka 2008, akiisaidia kushinda mataji sita ya LaLiga na matatu ya Ligi ya mabingwa Ulaya kwa kipindi cha mafanikio alichochea hapo.








# MOYO KUMSTAAFISHA SOKA AGUERO

**BARCELONA,** Hispania

SERGIO Aguero bado anasubiri kujua kama tatizo la moyo alilolipata hivi karibuni litamlazimisha kustaafu kucheza soka.

Ripoti kutoka viunga vya Katalunya ziliipasha Ijumaa kwamba, Aguero anaweza kulazimika kustaafu kucheza soka mapema, kwa sababu ya matatizo ya moyo yaliyomkumba.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alipatwa na tatizo la maumivu ya kifua kwa mara ya kwanza wakati Barca ikitoka sare dhidi ya Alaves Oktoba 30, ambapo klabu hiyo baadae ilibainisha kwamba, alipatwa na tatizo la mapigo ya moyo kubadilika kwa kasi.

Baada ya kufanyiwa vipimo, Aguero ambaye ameanza katika mechi mbili tu za LaLiga tangu atue hapo kwa uhamisho huru akitokea Manchester City, ilitangazwa kwamba atakuwa nje ya dimba kwa miezi mitatu.

Baadae redio Catalunya iliripoti kuwa tatizo lake ni kubwa zaidi tofauti na ilivyofikiriwa na Aguero anaweza kulazimika kutundika daruga katika umri wake wa miaka 33.

Hata hivyo, straika huyo wa zamani wa Atletico Madrid aliandika kwenye Twitter kukanusha taarifa hizo Ijumaa, akisema bado hatima yake haijajulikana na itajulikana Februari mwakani.



# Kane: Tulionesha shoo ya kibabe kwa Albania

**LONDON,** England

MFUNGAJI wa mabao matatu 'Hat-trick', Harry Kane, alikuwa na furaha wakati England ikiishushia kipigo cha kibabe Albania na kushinda 5-0 pale kwenye dimba la Wembley na kuweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya kufuzu kombe la Dunia mwakani nchini Qatar.

Mabao matano ya kipindi cha kwanza yaliwawezesha Simba Watatu hao kupata ushindi rahisi Ijumaa, na ikiwa na maana kwamba, kikosi hicho cha kocha, Gareth Southgate kinahiji pointi moja tu kutoka kwenye mchezo wao wa mwisho wa kundi I dhidi ya San Marino Jumatatu ili kufuzu.

Kane amekuwa akishutumiwa kutokana na kiwango kibovu klabuni kwake akiwa amefunga bao moja tu katika mechi 10 za Ligi Kuu ya England alizoichezea Tottenham Hotspur. Lakini Ijumaa alikuwa kwenye kiwango bora kabisa akiichezea nchini yake, akifunga mabao matatu 'hat-trick'.

Akizungumza na BBC Radio Five Live baada ya mchezo huo, Kane alisema: "(Ulikuwa) usiku bora kabisa kwa timu. Jambo la msingi zaidi ni ushindi ambao tuliupata bila tatizo.

"Kwenda kipindi cha pili tukiwa na uongozi wa 5-0 kwa hakika ilikuwa shoo ya kibabe kwa kikosi chetu.

"Hatukuwa na kiwango cha kuvutia kwenye mechi zilizopita katika uwanja wa Wembley na tulitaka kusahihisha makosa yetu na tulifanya hivyo.

# PRISONS YAIFUNGIA KAZI MBEYA KWANZA

Na Saada Akida

KOCHA Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shaban Kazumba, amesema walikuwa na upepo mbaya katika mechi tano za mwanzoni na sasa umeondoka na kikosi kimerejea katika ubora wake na wataanza rasmi Ligi Kuu Tanzania, dhidi ya Mbeya Kwanza.

**Prisons wanashuka dimbani Novemba 19, 2021, kuwakaribisha Mbeya Kwanza katika mchezo wa ligi hiyo utakaopigwa katika dimba la Nelson Mandela mkoani Rukwa.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kazumba alisema hawakuwa na mwanzo mzuri katika michezo mitano kwa kutoambulia ushindi, wamefanya kazi upungufu wao na wanatarajia kuanza ligi hiyo dhidi ya Mbeya Kwanza.

Alisema hawakuridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa kwenye mechi tano zilizopita, wiki mbili za mapumziko ya kalenda ya Fifa wamezitumia kufanyia kazi udhaifu wao na kupata mwelekeo mzuri.

"Tulikuwa na upepo mbaya katika mechi hizi tano za mwanzoni, tumefanyia kazi na sasa tunarudi katika ubora wetu dhidi ya Mbeya Kwanza kwa kuhakikisha tunapata pointi muhimu ili kujiondoa katika nafasi ya chini katika msimamo," alisema Kazumba.

Alisema ligi msimu huu imekuwa na ushindani mkubwa na ugumu mkubwa kwa sababu zote zimejiandaa vizuri na kila mmoja anapambana kutafuta matokeo mazuri na wao wamefanyia kazi na wako imara zaidi.

"Kwa sasa tunapigana timu yetu na upepo mbaya umepita kwa sababu tumeimarisha kikosi chetu na yoyote atakayekuja hatatoka salama katika uwanja wetu wa nyumbani," alisema Kazumba.

Prisons, imecheza mechi tano, sare mbili na imepoteza mechi tatu ikiwa na pointi 2, ikishika mkia katika msimamo wa Ligi Kuu.



Wachezaji wa Yanga wakifanya mazoezi ya mwisho kwenye kambi yao Visiwani Zanzibar kabla ya kurejea Dar es Salaam kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Namungo, utakaopigwa Novemba 20. Kikosi hicho kilirejea jana. **NA MPIGA PICHA WETU**

## Kocha DTB apania pointi 3 kwa Transit Camp

Na Saada Akida

KIKOSI cha timu ya DTB FC kinachoshiriki Ligi ya Championship zamani Ligi Daraja la kwanza, kitashuka dimbani leo kuwakaribisha Transit Camp kwenye uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

DTB FC imekuwa miongoni mwa timu tishio katika ligi hiyo imefanya usajili wa wachezaji wazoefu, akiwamo Amisi Tambwe ambaye amekuwa hatari wa kufumania nyavu.

Timu hiyo inayonolewa na Kocha Mkuu, Ramadhani Nsanzurwimo ambaye ni raia wa Burundi, aliyedhamilia kuhakikisha anapambana kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Kwa mujibu wa Kocha huyo, wamefanya maandalizi mazuri na ana imani na wachezaji wake kufanya vizuri katika michezo yao ikiwamo dhidi ya Transit Camp utakaopigwa leo.

Alisema wamejiandaa vizuri ana imani mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu timu zote zinataka kupata pointi tatu kwenye mchezo huo.

"Nina imani na wachezaji wangu, tumefanya maandalizi mazuri, hatuna mechi rahisi tunaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri, Transit Camp sio timu ya kuidharau, kwa sababu nao wamejipanga vizuri na kufanya usajili mzuri," alisema Nsanzurwimo.


LIVE IN PLAY

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA



PAKUA SASA

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 14 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1645 | Granada B vs UD Alzira | 1.89 | 3.14 | 3.96 |
| 13:30 | 2505 | Pd Santa Eulalia vs CD Teruel | 2.15 | 3.04 | 3.28 |
| 14:00 | 1708 | Atl Mancha Real vs Levante B | 2.67 | 2.86 | 2.67 |
| 14:00 | 4790 | Deportivo La Coruna vs UD Extremadura | 1.44 | 3.70 | 7.31 |
| 14:00 | 4967 | San Sebastian Reyes vs Zamora CF | 2.35 | 2.99 | 2.94 |
| 14:00 | 5102 | UD Montijo vs Cadiz B | 2.09 | 2.84 | 3.71 |
| 14:30 | 2902 | Khon Kaen United FC vs Bangkok Utd | 5.39 | 4.33 | 1.46 |
| 15:30 | 2496 | Jadran Dekani vs NK Dob | 2.70 | 3.42 | 2.29 |
| 15:30 | 2632 | NK Rogaska vs ND Primorje | 2.55 | 3.42 | 2.41 |
| 15:30 | 2720 | Krka vs Rudar Velenje | 2.32 | 3.42 | 2.65 |
| 16:00 | 5094 | Amorebieta vs Lugo | 2.04 | 3.14 | 3.68 |
| 16:30 | 3127 | De Graafschap vs Telstar | 1.41 | 4.59 | 6.24 |
| 16:30 | 3229 | Palermo vs Potenza SC | 1.64 | 3.66 | 5.34 |
| 16:30 | 5823 | Pro Vercelli vs Legnago | 1.75 | 3.47 | 4.77 |
| 17:00 | 1741 | Brighton and Hove Albion W vs Leicester City FC W | 1.42 | 4.51 | 5.76 |
| 17:00 | 2202 | Thisted FC vs Aarhus Fremad | 2.24 | 3.61 | 2.65 |
| 17:00 | 2249 | Slovenia vs Cyprus | 1.31 | 4.89 | 10.98 |
| 17:00 | 2355 | Catania vs Foggia | 2.32 | 3.18 | 3.08 |
| 17:00 | 3906 | Malta vs Slovakia | 7.19 | 3.75 | 1.53 |
| 17:00 | 4368 | Croatia vs Russia | 1.59 | 3.99 | 5.59 |
| 18:00 | 1639 | Girona vs FC Cartagena | 1.69 | 3.49 | 4.92 |
| 18:00 | 4511 | UD Ibiza Eivissa vs Almeria | 3.24 | 3.19 | 2.18 |
| 18:30 | 2637 | Izarra vs Racing Rioja CF | 2.65 | 3.18 | 2.45 |
| 18:45 | 1230 | ADO Den Haag vs VVV Venlo | 1.78 | 3.81 | 3.86 |
| 19:00 | 1787 | CD Badajoz vs UD Logrones | 2.54 | 2.93 | 2.74 |
| 19:00 | 3363 | Assyriska vs Umeaa FC | 4.10 | 4.10 | 1.73 |
| 19:00 | 5627 | Real Murcia vs CD Eldense | 1.84 | 3.18 | 4.14 |
| 19:30 | 3779 | Messina FC vs Avellino | 2.98 | 3.13 | 2.41 |
| 19:30 | 3895 | Bari vs Vibonese Calcio | 1.32 | 4.74 | 9.68 |
| 19:30 | 4028 | Aquila 1902 Montevarchi vs Imolese Calcio | 2.53 | 3.12 | 2.82 |
| 19:30 | 4169 | AZ Picerno vs Virtus Francavilla | 2.45 | 3.07 | 2.97 |
| 19:30 | 4464 | Paganese vs Fidelis Andria | 2.02 | 3.13 | 3.92 |
| 19:30 | 4920 | Monopoli vs Taranto Sport | 2.07 | 3.07 | 3.82 |
| 19:30 | 5758 | Virtus Entella vs Grosseto | 1.59 | 3.75 | 5.73 |
| 19:30 | 5932 | Juve Stabia vs Nuova Monterosi | 1.79 | 3.42 | 4.56 |
| 20:00 | 1371 | Armenia vs Germany | 15.40 | 7.53 | 1.16 |
| 20:00 | 2218 | Liechtenstein vs Romania | 24.04 | 8.41 | 1.11 |
| 20:00 | 4725 | North Macedonia vs Iceland | 1.57 | 4.00 | 5.80 |
| 20:15 | 4245 | Burgos vs Ponferradina | 2.35 | 2.94 | 3.18 |
| 20:15 | 5533 | Leganes vs Real Oviedo | 1.99 | 3.10 | 3.94 |
| 22:00 | 3145 | Estudiantes FC vs Deportivo Tachira | 2.74 | 3.41 | 2.26 |
| 22:00 | 4193 | Deportes Quindio vs Patriotas FC | 1.85 | 3.27 | 3.95 |
| 22:00 | 4787 | CD Palestino vs Cobresal | 1.81 | 3.62 | 3.67 |
| 22:00 | 5180 | SBV Excelsior vs Almere City | 1.99 | 3.72 | 3.18 |
| 22:00 | 5614 | Ghana vs South Africa | 1.78 | 3.14 | 4.55 |
| 22:00 | 5961 | Sao Paulo vs Flamengo | 3.03 | 3.08 | 2.25 |
| 22:45 | 3773 | Luxembourg vs Ireland | 3.60 | 3.15 | 2.15 |
| 22:45 | 3787 | Portugal vs Serbia | 1.38 | 4.79 | 7.98 |
| 22:45 | 3854 | Greece vs Kosovo | 1.65 | 3.74 | 5.39 |
| 22:45 | 3977 | Spain vs Sweden | 1.38 | 4.51 | 8.63 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Novemba 14, 2021

Nipashe




Barca yamsajili tena Alves

UKURASA 21



Nahodha wa timu ya taifa ya England, Harry Kane (kushoto), akifunga bao lake la tatu na la tano kwa timu hiyo dhidi ya Albania wakati wa mchezo wa kufuzu kombe la Dunia mwakani nchini Qatar, mchezo uliopigwa uwanja wa Wimbley jijini London, juzi. England ilishinda 5-0. **PICHA: MTANDAO**

# NABI AZICHAMBUA MECHI 'TATA' BARA

## ●●● Afunguka ni lazima wapate ushindi ili...

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi chake kikiendelea kusaka makali huko Visiwani Zanzibar, Kocha Mkuu wa Yanga, Nassredine Nabi, amesema mechi nne zinazofuata za timu yake katika mwendelezo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara zinamnyima 'usingizi'.

**Ikiwa Zanzibar, Yanga imeshacheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya KMKM na Mlandege, zote za visiwani huko.**

Mechi zinazofuata za Yanga zitakuwa ni dhidi ya Namungo FC itakayochezwa Novemba 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi halafu itawafuata Mbeya Kwanza ifikapo Novemba 30 na baada ya mchezo huo itarejea jijini Dar es Salaam kuwavaa watani zao Simba hapo Desemba 11, mwaka huu.

Mtihani wa nne utakuwa ni dhidi ya Tanzania Prisons ambayo itachezwa Desemba 19, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema mechi za kirafiki walizocheza Zanzibar zimemsaidia kukiimarisha kikosi chake na anaamini kitaendeleza kasi ya ushindi waliyoanza nayo msimu huu wa 2021/22.

Nabi alisema alihitaji muda zaidi wa kukiweka 'sawa' kikosi chake na mapumziko ya mechi za kimataifa waliyopata kwake yamekuwa ni 'neema'.

"Mechi nne zinazofuata zinanipa 'mawazo', kichwa changu kinafikiria sana kuhusu mechi hizo, tunahitaji kuendelea na maandalizi maalum kwa ajili ya kuwa fiti kupambana na wapinzani wetu," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema kwake ratiba hiyo ni ngumu na ndio sababu ya msingi ya kuhitaji kambi na mechi za kirafiki ili kufikia malengo.

"Ninahitaji kupata matokeo mazuri, kwangu ninaiona ratiba ni ngumu na ya mtego, inaniumiza kichwa, nimeandaa programu maalumu ambayo itatusaidia kupata matokeo mazuri katika michezo hiyo na kuendelea kuongoza ligi," Nabi alisema.

Aliongeza timu ambazo watakutana nazo ni bora na kila upande hauhitaji kupoteza pointi hasa kwenye mechi muhimu za mzunguko wa kwanza.

"Nimewaona Namungo, wanacheza kwa kuzuia, ili upate matokeo kwao ni lazima uingine na mfumo tofauti ambao hawajauzoea, hii ndiyo Yanga ambayo ninahitaji kuwa nayo, mechi zote ni ngumu na mimi jukumu langu ni kuhakikisha naandaa ufumbuzi," alisema kocha huyo.

Hata hivyo Nabi aliwapongeza tena wachezaji wake kwa kuwa timu pekee ambayo imepata ushindi katika mechi zote tano walizocheza kwenye ligi hiyo ya juu lakini amewakumbusha hawatakiwi kuwadharau wapinzani.

"Katika mechi za kirafiki huku Zanzibar nimebadilisha baadhi ya wachezaji, nimewapa pia nafasi wale ambao hawana namba, wamenifurahisha, naamini wanaweza kupambana sasa kuingia kwenye kikosi cha kwanza cha timu na hii itaongeza ubora wa timu," aliongeza.

Alisema pia licha ya kuwakosa wachezaji walioko kwenye majukumu ya kimataifa, bado nyota walioko Zanzibar wamepambana na kuipa klabu heshima ya kuonyesha viwango vya juu.

"Kwa sasa tumeanza kufanyia kazi ubora na madhaifu ya Namungo, ni timu ngumu, inatumia nguvu sana, nafahamu watakupokuwa nyumbani watakuwa wagumu zaidi, tutajipanga vizuri kukabiliana nao," aliongeza.

Novemba 3, mwaka huu, Nabi alikuwa uwanjani kushuhudia Simba ikipambana na Namungo, ambapo dakika 90 zilimalizika kwa mabingwa watetezi kupata ushindi wa bao 1-0, mfungaji akiwa ni Meddie Kagere.

## Stars kulinda heshima leo

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuondolewa kwenye kinyang'anyiro cha kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia nchini Qatar mwakani, timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, leo inashuka dimbani kwenye Uwanja wa Kianja Barea Mahamasina, jijini Antananarivo, kucheza dhidi ya Madagascar.

Licha ya kwamba ni mechi ya kukamilisha ratiba, Stars imeonekana kulichukulia uzito pambano hilo, kwakuwa mbali na kulinda heshima, kama ikishinda itaongeza pointi kwenye viwango vya soka vya nchi.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, amesema kuwa lengo ni kupata ushindi licha ya kwamba Stars haiwezi kwenda Qatar.

Kuhusu kufungwa, alisema matokeo hayakufurahiwa na mashabiki tu, bali hata wachezaji wenyewe kwa sababu nia yao ilikuwa ni kushinda ili kufuzu fainali hizi, lakini kilichotokea ndiyo soka.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >